

VITABU VYA MANABII

Kitabu 3

*Mafundisho juu ya
EZEKIELI
na DANIELI*

Mwandishi : ELEZOHAKI

Everyday Publications Inc
310 Killaly St. West
Port Colborne, ON
Canada L3K 6A6

Soma maneno haya

Kitabu hiki cha mafundisho juu ya unabii wa Ezekieli na Danieli ni kitabu cha tatu juu ya vitabu vine vya Manabii katika Agano la Kale.

Kitabu cha kwanza ni juu ya unabii wa Isaya.

Kitabu cha pili ni juu ya Yeremia na Maombolezo.

Vizuri ujipatie na kusoma kitabu cha kwanza na cha pili, ndi-
vyo mafundisho juu ya Isaya na Yeremia na Maombolezo kama
usipovisoma bado. Vitakusaidia kufahamu vitabu vingine vya
unabii vilevile.

Soma sura moja ya Ezekieli au Danieli kila siku pamoja na
kitabu hiki kwani si faida kusoma kitabu hiki peke yake. Sharti
ukisome pamoja na Biblia. Ni lazima vilevile kusoma ndani ya
Biblia yako mashairi yote mengine ambayo kitabu hiki kinataja.

Kwa mwisho wa mafundisho juu ya sura nyingine utaona
ulizo. Jaribu kujibu maulizo haya, kisha angalia kwa kurasa 47 na
48 kuona kama ulijibu vizuri.

ISBN 978-0-88873-104-3

Imprimé au Canada

EZEKIELI

1. Mungu aliita Ezekieli na alimtuma kuhubiri kwa watu wa ufalme wa Yuda, ndiyo makabila ya Yuda na Benyamina

1:13:21

1. Mungu alionyeshea Ezekieli ono la utukufu wake, 1:1-28
2. Mungu aliagiza Ezekieli kuhubiri kwa watu wa Yuda, 2:1-3:21
 - 1) Watu waliasi Mungu saa zote, 2:1-7
 - 2) Ezekieli aliagizwa kuwalishya ya kwamba Mungu atawahukumu, 2:8-3:3.
 - 3) Wayuda walikuwa watu wa namna gani, 3:4-11.
 - 4) Nabii Ezekieli alikuwa kama zamu anayelinda inchi yake, 3:12-21.

2. Ezekieli alionyeshea watu wa Yuda na Yerusalem ya kwamba Mungu atawahukumu

3:22-24:27

1. Mungu aliagiza Ezekieli kunyamaza kimya na kujulisha watu habari zake kwa njia ya matendo yake kufika saa Mungu atakapomwagiza kusema tena, 3:22-27.
2. Ezekieli alitumika na tofali la dari kuonyesha ya kwamba majeshi ya adui watapiga vita na watu wa Yerusalem, sura 4.
3. Ezekieli alitumia upanga mkali kukata nyele zake mwenyewe kama mfano kuonyesha ya kwamba Mungu atahukumu Yuda, sura 5.
4. Bwana ataharibu miungu migeni lakini ataokoa watu wachache inchini mwa Yuda, sura 6.
5. Majeshi ya Babeli watafika nyuma kidogo na kupiga vita na Yerusalem, sura 7.
6. Mungu alionyeshea Ezekieli ya kwamba watu wa Yuda walikuwa wakiabudu sanamu ndani ya hekalu la Bwana, sura 8.
7. Bwana ataondokea hekalu lake na ataharibu watu wale wailioabudu sanamu, sura 9.

4 EZEKIELI

8. Mungu atafikia Yerusalem na kuuhukumu, sura 10.
 9. Mashauri ya wakubwa waovu yatahindwa, 11:1-13.
 10. Mungu aliahidi kurudisha wengine wa watu kwa inchi yao, 11:14-21.
 11. Wingu la utukufu lilipanda na kusimama juu ya Mlima wa Mizeituni, 11:22-25.
 12. Ezekieli aliondosha vitu vyake nyumbani mwake kama mfano kuonyesha ya kwamba Waisraeli watakwenda Babeli kama wafungwa, sura 12.
 13. Manabii wa uwongo watahukumiwa, sura 13.
 14. Mungu alijulisha watu wale walioabudu sanamu ya kumba atawahukumu, sura 14.
 15. Ufalme wa Yuda ulikuwa kama mzabibu lakini utateketezwa wakati Wababeli watakapowafikia, sura 15.
 16. Ezekieli alisema tena ya kwamba watu wa Yerusalem hawakuwa waaminifu kwa Bwana, sura 16.
 17. Mezali kuonyesha kwamba watu wa Yuda watageuka wafungwa, sura 17.
 18. Mifano kuonyesha namna Mungu anavyohukumu watu wote kwa haki, sura 18.
 19. Maombolezo kwa wafalme wa mwisho wa Yuda, sura 19.
 20. Waisraeli walikuwa wameasi Mungu mara nyingi, 20:1-31.
 21. Mungu alikusudi kutawala juu ya watu waliokwisha kusafishwa, 20:32-44.
 22. Majeshi ya Babeli watapita juu ya Yuda kama moto wa kuogopesha unavyoteketeza mto, 20:45-21:32.
 23. Watu wa Yerusalem walikuwa wamefanya zambi na itapasa Mungu kuwaazibu, sura 22.
 24. Mezali juu ya miji miwili iliyotenda kama kahaba, sura 23.
 25. Mezali juu ya sufuria iliyotokota, 24:1-14.
 26. Ezekieli alieleza kwa nini alitenda namna nyingine, 24:15-27.
- 3. Ezekieli alipasha namna Mungu atakavyoazibu mataifa saba,** **25:1 – 32:32**
1. Amoni, 25:1-7

2. Moabu, 25:8-11
 3. Edomu, 25:12-14
 4. Filistia, 25:15-17
 5. Tiro, 26:1-28:19
 6. Sidoni, 28:20-26
 7. Misri, 29:1-32:32
- 4. Mungu alikusudi kurudisha Waisraeli karibu naye na kuazibu adui zao zote sura 33 – 39**
1. Mungu aliweka Ezekieli tena kuwa zamu, kuonya watu, sura 33.
 2. Wachungaji wabaya na Mchungaji mwema, sura 34.
 3. Mungu atahukumu watu wa Edomu, sura 35.
 4. Mungu atarudisha Israeli kwa inchi yao wenyewe, sura 36.
 5. Ono la mifupa iliyokauka bondeni, 37:1-14.
 6. Miti midogo miwili ilikuwa mfano wa namna Mungu atakavyofunganisha Israeli na Yuda pamoja tena, 37:15-28.
 7. Mungu ataharibu adui za Israeli kwa wakati wa kuja, sura 38-39.
- 5. Miaka 1000 ya baraka sura 40 – 48**
1. Hekalu litajengwa tena kwa Yerusalem, sura 40-44.
 2. Waisraeli watacaa inchini mwao wenyewe, na Kristo atatalawa kama Mfalme, sura 45-48.

Ezekieli alikuwa kuhani, mwana wa Buzi (1:3). Maana ya jina lake ni *Mungu ananipatisha nguvu*. Alikaa mjini mwa Yerusalem lakini alipelekwa kwa Babeli wakati mfalme wa Babeli alipotuma majeshi yake mara ya pili kupiga vita na Yerusalem, miaka 11 mbele ya kuharibu Yerusalem kabisa.

Kwa Babeli Ezekieli alikaa pamoja na Wayuda wengine walio-pelekwa pale na Nebukadneza, na aliwafundisha Neno la Mungu kwa miaka 27. Wayuda walifikiri watarudi kwa inchi yao nyuma kidogo lakini Ezekieli aliwaambia ya kwamha iliwapasa kurudi kwanza karibu na Bwana.

Kitabu cha Ezekieli kina sehemu tatu. Kwanza nabii aliku-mbusa watu zambi za watu wa Yuda na aliwaonya ya kwamba Mungu atawahukumu nyuma kidogo. Adui zao wataharibu mji wa Yerusalem na kupeleka watu pahali pengine kama wafu-

6 EZEKIELI

ngwa. Ezekiel aliwajulisha maneno baya kwa njia ya kuwapasha habari za maono ya ajabu ambayo aliona. Alitenda namna nyingine ya namna watu wanavyotendaga kufundisha watu waliomwangalia. Aliona wingu la kungaa juu ya hekalu. Wingu hili lilionyesha ya kwamba Mungu alikuwa pamoja na watu wake. Lakini Wayuda walimkosea, hivi ilimpasa kuondoka katikati yao. Wingu lilihama polepole; neno hili lilionyesha ya kwamba Mungu hakutaka kuondoka lakini alilazimishwa kufanya hivi. Walikuwa wamechafua hekalu na zambi zao, na wengi wao watakuwa wakati Mungu atakapotuma adui kuwaharibu.

Ndani ya sehemu ya pili ya kitabu hiki Ezekieli alitabiri ya kwamba Mungu ataazibu mataifa waliozunguka inchi ya Israeli. Walikuwa waabudaji sanamu na walitendea watu wa Israeli kwa ukali sana. Ndani ya sura hizi Ezekieli aliandika juu ya watu wa Amoni, Moabu na Edomu, juu ya Wafilistini na Tiro, Sidoni na Misri.

Halafu ndani ya sehemu ya mwisho ya kitabu chake Ezekieli alipasha juu ya wakati Mungu atakapokutanisha watu wa Israeli na Yuda pamoja tena ndani ya inchi yao, ndiyo inchi ya Palestina. Watu wataacha zambi zao na Mungu ataweka Roho Mtakatifu yake ndani yao. Masiya, ndiye Bwana Yesu Kristo, atafikia watu wake na ataharibu adui zao za mwisho. Watajenga hekalu tena na utukufu wa Bwana utalirudia. Unabii huu haujatimizwa bado; utatimizwa kwa wakati wa utawala wa Kristo duniani kwa miaka elfu moja.

Maneno tunayosoma ndani ya kitabu cha Ezekieli hayafulatani. Mara nyingine tunasoma juu ya maneno yaliyotokea nyuma mbele ya yale yaliyotokea kwanza. Ni vivyo hivyo ndani ya vitabu vingine vya manabii. Shairi la kwanza la sura nyingi linapasha kama habari za sura ile zilitokea wakati gani.

*Nebukadneza, mfalme wa Babeli alishinda
wawafalme wa Yerusalem*

- | | | |
|-------------|--------------------|------------------|
| 1. Yoyakimu | 2 Wafalme 24:1-2 | 2 Mambo 36:6-7 |
| 2. Yoyakinu | 2 Wafalme 24:10-16 | 2 Mambo 36:9-10 |
| 3. Zedekia | 2 Wafalme 25:1-17 | 2 Mambo 36:11,17 |

SURA 1

Ezekieli aliandika sura 1-24 za unabii wake wakati Nebukadneza asipoharibu Yerusalem bado. Alikuwa mfungwa inchini mwa Babeli lakini alitangaza ya kwamba Yerusalem utakamatwa na adui na kuteketezwa miaka sita au saba mbele ya kutokea kwa neno hili. Tunafikiri Ezekieli alikuwa na miaka karibu 30 wakati alipoanza kuandika (1:1).

Sura ya kwanza inapasha juu ya ono la utukufu wa Mungu ambalo Ezekieli aliona. Aliona viumbe hai wane. Kila kiumbe alikuwa na nyuso ine (uso wa simba, wa ngombe ndume, wa tai na wa mtu). Kila kiumbe alikuwa na mawingu mane, miguu alima na mikono chini ya mabawa yake. Aliona gurudumu kando ya kila kiumbe na ndani ya kila gurudumu kulikuwa na gurudumu lingine. Magurudumu haya yalikwenda kila pahali viumbe vilipokwenda. Ezekieli aliona kitie cha kifalme vilevile na Bwana wa utukufu akikaa juu yake. Aliona ono hili la utukufu wa Mungu na nyuma yake Mungu alimwita kumtumikia kama nabii.

Kuna maneno mengine ndani ya sura hii yaliyo nguvu kwa sisi kufahamu lakini mafundisho yake makubwa ni wazi. Roho Mtakatifu anatupa sisi hapa mfano wa kushangaza wa utukufu wa Mungu. Hakuna mtu aliyeona Mungu na macho wakati wo wote (Yoane 1:18), lakini sura hii inatufundisha ya kwamba yeze ni mkubwa sana.

Mungu alionyeshea Ezekieli nini mbele ya kumwita kuwa nabii?

SURA 2

Mungu alijua ya kwamba taifa la Yuda hawatamii, lakini aliagiza Ezekieli kutabiri kwa masikio yao hata kama wakikataa kusikiliza. Haifai Ezekieli kuwaogopa lakini kutii Mungu. Kisha Mungu alimwagiza kula kitabu kidogo. Ndani ya kitabu hiki ziliandikwa habari za azabu Mungu atakayotuma juu ya taifa la Yuda.

Taja manabii wawili wengine walikula maneno ya Mungu (Yeremia 15:16; Ufunuo 10:10).

SURA 3

Ezekieli alikula kitabu kama Mungu alivyomwagiza kufanya

8 EZEKIELI

(mash.1-3). Halafu Mungu alisema tena ya kwamba alituma Ezekieli karibu na watu watakaokataa kusikia. (Watu wa Yuda wanaitwa Israeli hapa.) Haifai Ezekieli aogope kusema kwa watu waliokaa kwanza inchini mwa Yuda, au kwa wale waliokuwa wafungwa inchini mwa Babeli (mash. 4-11). Kisha Bwana alipeleka Ezekieli karibu na Wayuda waliokuwa kwa mto Kebari karibu na mji wa Babeli na Ezekieli alikaa pamoja nao kwa siku saba (mash.12-15).

Mungu aliweka Ezekieli kuwa mlinzi au zamu na kumpa kazi ya kuonya watu (mash.16-21). Nyuma yake Ezekieli aliagizwa kwenda kwa nyumba yake pahali atakapofungwa na kamba. Hataweza kusema neno kufika wakati Mungu atakapomjulisha nini itampasa kusema (mash. 22-27).

Mungu aliweka Ezekieli kuwa zamu kuangalia na kujulisha watu kama adui walikuwa wakikaribia. Alimwagiza kuonya waovu ya kwamba watahukumiwa. Bwana Yesu Kristo alionya watu waliokaa ndani ya miji miovu (Matayo 11:20-24). Petro aliagiza watu wa Yerusalem kutubu (Matendo 2:36,38). Ingetupasa sisi kufanya vivyo hivyo.

Kwa njia gani Ezekieli alikuwa kama zamu?

SURA 4

Kisha Mungu aliagiza Ezekieli kutenda maneno yatakayoleta watu kufikiri juu ya vita kwa Yerusalem. Ezekieli aliagizwa kukamata tofali na kutumika nalo kama mfano wa mji. Chungu cha chuma ilikuwa mfano wa ukuta uliogawa Ezekieli na mji na kumzuiza asisaidie watu mjini (mash.1-3). Nabii aliagizwa kulala kwa mbavu zake za kushoto siku 390 kwa watu wa Israeli na kwa mbavu zake za kuume siku 40 kwa watu wa Yuda. Siku moja ilikuwa mfano wa mwaka mmoja lakini hatujui maana ya muda hizi. Mashairi 9-17 yanapasha juu ya njaa kubwa ya watu wakati jeshi la Wababeli lilipokuwa likizunguka mji. Kila mtu atapewa vyakula na maji nusu tu na watu watatumika na mavi ya ngombe kama kuni kupika vyakula vyao.

Kwa nini Ezekieli alilala kwa mbavu zake kwa siku nyingi?

SURA 5

Ezekieli alionyesha mfano mwingine kwa watu. Aliteketeza sehemu moja ya tatu ya nyele zake kwa moto kuonyesha ya kwamba sehemu moja ya tatu ya watu katika Yerusalem wata-pata ugonjwa gafula na watakufa. Alikata sehemu ya tatu nyingine ya nyele zake vipande vipande na kisu kuonyesha ya kwamba sehemu moja ya tatu ya watu watauawa kwa upanga vitani. Zaidi ya baki la watu watasambazwa kwa inchi nyingine (mash. 2,12). Watu wachache wataachwa katika Yerusalem laki-ni hata wengine wa watu hawa watauawa (mash.3,4). Maneno haya ya kuogopesha yatapata Yerusalem kwa sababu ya zambi za watu. Walibarikiwa kupita mataifa waliokaa kando kando yao lakini walikuwa waovu zaidi (mash. 5-9). Wakati vyakula vita-kapokwisha mjini wengine wao watakula hata miili ya watu wengine (sh.10). Wayuda walikuwa wamechafua hekalu na Mungu hatawahurumia (mash. 11-13). Watu wa mataifa mengine watazarau Wayuda, watawatendea kwa ukali na kuua wengine katikati yao (mash. 14-17).

Mungu aliagiza Ezekieli kukata nyole zake kwa sababu gani?

SURA 6

Mungu aliagiza Ezekieli kutabiri ya kwamba milima ya Israeli itahukumiwa kwa sababu mara nyingi watu walismamisha sana-mu zao juu ya milima (Hosea 4:13). Mungu atahukumu inchi ya Israeli kwa sababu watu waliabudu sanamu (mash. 1-7). Watu wachache tu watapona na watakumbuka Bwana wakati wata-kapokuwa kwa Babeli. Watajichukia wenyewe kwa sababu ya maneno maovu waliyokwisha kufanya (mash. 8-10). Bila shaka Mungu atahukumu baki la watu kwa sababu ya kuabudu sana-mu; atatuma tauni, vita na njaa kali (mash. 11-14).

Mungu aliumba roho wengi mbele ya kuumba watu. Alitaka roho hawa kumtumikia lakini wengine wal-imwasi. Mungu anataka watu kumpenda na ku-mwabudu lakini watu wote wamemgeukia. Wengi wanaabudu sanamu na mashetani (1 Wakorinto 10:20). Kwa pahali pa kutumikia Mungu wanatumikia roho walioasi Mungu. Ni kazi yetu kupasha watu wote habari za Mungu wa kweli (Matendo 14:15).

SURA 7

Saa ilikuwa imetimia na Mungu alikuwa karibu kutuma hukumu yake, na watu wote watajua ya kwamba hukumu hii ilitoka kwa Bwana (mash. 1-13). Wakubwa wataita watu wao kupiga vita lakini wao wote watakataa kutii. Watu wengine walikuwa wameuawa, na watu waliobaki walikuwa zaifu na waliogopa (mash. 14-18). Mali yao haitawasaidia (sh.19). Hekalu la Mungu lilikuwa na mapambo mengi lakini watu walikuwa wamelichafua kwa njia ya kuweka sanamu zao ndani yake. Kwa sababu hii Mungu atatoa hekalu mikononi mwa wageni, ndio Wababeli watakaoiba vitu vya bei gali vilivyokuwa ndani yake na kuliharibu (mash. 20-22). Watu namna zote watataabishwa, mfalme na wana wake, manabii, wazee wa watu na watu wote (mash. 23-27).

SURA 8

Sasa Bwana alisaidia Ezekieli kuona maneno yaliyokuwa yakifanyikana ndani ya hekalu kwa Yerusalem hata kama hakuwa pale ye ye mwenyewe. Ezekieli aliona:

1. sanamu ya kuogopesha pale pale ndani ya hekalu. Bwana ye ye mwenyewe alikuwa pale vilevile naye alikuwa na vivu juu ya sanamu ile (mash. 1-3) na alihuzunishwa sana kwa sababu ya neno hili ovu mbalo watu wake walikuwa wamefanya (mash. 4-6) .
2. Neno la pili nabii aliloona lilikuwa kiwanjani mwa hekalu. Wazee wa Yuda walikusanya pale na kuabudu picha ovu juu ya viambaza (mash. 7-13).
3. Neno la tatu lilikuwa kwa langa la kaskazini: wanawake walikuwa wakiabudu Tamusi, mmoja wa miungu ya Wababeli (mash. 14-15).
4. Kisha Ezekieli aliona waabudaji sanamu hata ndani ya kiwanja cha ndani cha hekalu. Wanaume 25 walikuwa pale wakiabudu jua na kufanya maneno machafu yote ambayo waabudu jua wanafanya (mash. 16-18).

Ezekieli alikuwa nabii na kuhani vilevile. Ilikuwa kazi ya makuhani kuzuiza watu waovu wasiingie hekaluni. Hata mfalme mmoja alifikuzwa toka hekalu na makuhani (2 Mambo 26:20). Mungu alionyeshea

Ezekieli maneno haya aweze kufahamu kwa nini ilikuwa lazima kwa Mungu kuharibu hekalu lake mwenyewe. Kumbuka ya kwamba ni sharti kwa Mungu kuhukumu zambi zote.

Ezekieli aliona zambi mbaya gani hata ndani ya hekalu takatifu la Mungu?

SURA 9

Ndani ya sura hii Ezekieli aliona malaika sita kama watu waliokuwa tayari kuua watu wale waliokuwa wakiabudu sana-mu ndani ya sura 8. Walitoka kwa kaskazini, kama Wababeli watakavyofanya. Wingu la utukufu lilihakikisha ya kwamba Mungu alikuwa pamoja na watu wake, lakini sasa wingu lili-ondokea pahali patakatifu sana hekaluni kwa sababu Mungu hawezi kukaa pamoja na sanamu. Wingu la utukufu lilihamma hata langa la mbele la kiwanja cha hekalu na kungaa kwake kulijaza kiwanja cha hekalu na nuru (sh.3). Wengine wa Wayuda walikaa kufuata Mungu nao walikuwa wamejaribu kuzuiza Wayuda wengine wasiabudu sanamu. Kwanza Wayuda hawa waaminifu walitiwa alama juu ya nyuso zao kusudi wasiuawe (sh.4). Kisha malaika sita walianza kuua waabudaji sanamu, wakianza na wanaume wazee waliokuwa viongozi (mash. 5-7). Ezekieli aliombea waabudaji sanamu hawa lakini Bwana alikataa kuwarehemu na kuwaachilia (mash. 8-11).

Mungu alikataa kujibu ombi la Ezekieli?

SURA 10

Sura hii inatupasha maneno mengine juu ya kiti cha kifalme na juu ya utukufu wa Bwana kupita yale tuliyosoma ndani ya sura 1. Hapa viumbe hai wanaitwa makerubi.

Ndani ya 9:2-3 tulisoma juu ya mtu mwenye mavazi ya kitani. Sasa Bwana aliagiza mtu huyu kutwaa makaa yaliyowaka kwa moto toka katikati ya makerubi na kuyasambaza juu ya Yerusalem (mash. 1,2). Neno hili lilikuwa mfano wa hukumu Mungu atakayomwanga juu ya mji. Mashairi 3-5 yanapasha tena juu ya kuhama kwa wingu la utukufu, kama tulivyosoma ndani ya 9:3. Halafu Ezekieli alipasha maneno mengine juu ya makerubi na magurudumu (mash. 6-17), lakini ni nguvu kufahamu kama

12 EZEKIELI

mambo haya yalioneckana namna gani. Halafu wingu la utukufu lilihamma toka kizingiti hata lango la mashariki la hekalu (mash.18-19). Ezekieli alisema wazi ya kuwa makerubi ndio viumbe hai ambavyo aliona ndani ya sura 1 karibu na mto Kebari.

SURA 11

Watu 25 walisema na watu wa mji ya kwamba hawahitaji ku-ogopa (mash. 1-3). Hatujui kabisa maana ya masemo yao lakini ni wazi ya kwamba walikuwa wakikana maneno Bwana aliokwisha kusema. Ezekieli aliagizwa kutabiri ya kuwa Bwana atahukumu Yerusalem bila huruma (mash. 4-12). Labda Pelatia alikuwa kiongozi cha watu wale 25. Wakati alipoanguka mufu, Ezekieli aliombea watu wake (sh.13). Mungu alimwambia ya kwamba atalinda watu wale waliopelekwa kwa inchi nyingine kama wafungwa na atawarudisha tena kwa inchi yao wenyewe. Kisha atawasafisha toka zambi ya kuabudu sanamu (mash. 14-21). Kwa mwisho wa sura hii, wingu la utukufu lilipanda toka mji na lilikwenda kwa Mlima wa Zeituni kwa upande wa mashariki wa Yerusalem (mash.22-25).

Wingu la utukufu halikuondokea hekalu gafula lakini pole-pole, kama Mungu hakutaka kuliondosha. Pahali pa kukaa pa wingu hili palikuwa hekaluni (8:4); lilihamma hata mlango wa mbele wa hekalu (9:3); halafu lilipita kwa langu la mashariki (10:19), na mwishoni kwa mlima kwa upande wa mashariki wa mji (11:23). Mungu alipenda watu wake hata kwa wakati ule lakin aliondokea mji na hekalu lake na hatarudi kufika wakati hekalu jipyä litakapojengwa saa Bwana atakapokuja tena (43:2).

Tunaona ya kwamba Muugu ni mtakatifu na anakataa kuacha watu kuendelea ndani ya zambi zao. Atahukumu watu wake mwenyewe mbele ya kuhukumu wenye zambi (1 Petro 4:17).

Wingu la utukufu lilihukia hekalu wakati gani? Ona 1 Wafalme 8:10.

SURA 12

Mungu aliagiza Ezekieli kuhamisha vitu vyake vyote toka nyumba yake na kuvipeleka pahali pengine. Hii ilikuwa alama kwa Wayuda ya kwamba itawapasa kuhama toka Yerusalem na

kwenda Babeli (mash. 1-7). Ezekieli alitoboa ukuta usiku na kwa njia hii alitabiri ya kwamba Mfalme Zedekia (anayetwa "mkubwa" ndani ya shairi 10) atakimbia mji usiku wakati asipoweza kuona inchi (mash. 8-12). Lakini adui watamkamata na kumpeleka kwa Babeli hata kama hataona inchi ile na macho yake mwenyewe (sh.13). Neno hili lilitokea kweli. Wababeli walikamata Zedekia wakati alipokimbia toka Yerusalem. Waliondoshya macho yake na kumpeleka kwa Babeli (2 Wafalme 25:7). Watu wasasambazwa katikati ya mataifa na wengi wao watakufa vitani. Wengine watakufa kwa njaa, au kwa tauni (mash. 14-16). Ezekieli alitetemeka wakati alipokula na kunywa—ndio mfano wa watu wa Yerusalem wakiogopa Nebukadneza wakati asipowapeleka bado kwa Babeli (mash. 17-20). Watu walikuwa wamesema ya kwamba Mungu hatafanya kamwe maneno Ezekieli aliyotabiri, lakini Ezekieli alisema siku ilikuwa imekaribia wakati maneno haya yote yatakaptimizwa na kila unabii au ono litakapofanyiana. Wengine walisema Mungu atatimiza maneno haya kwa wakati wa kuja lakini watu wale wataona hukumu ya Mungu hata kwa wakati wao wenyewe walipokuwa kwanza hai (mash. 21-28).

Mungu aliomba Ezekieli kufanya maneno namna nyingine kabisa aweze kufundisha na kuonya watu. Anataka sisi kuonyesha mapendo kwa watu wengine na kuwatangazia habari za Bwana Yesu. Mara nyingine ni nguvu kufanya hivi, lakini labda watu wengine wataokolewa.

SURA 13

Sasa Ezekieli aliandika juu ya manabii ya uwongo. Wengine walikuwa wanaume (mash. 1-16) na wengine wanawake (mash. 17-23). Walitunga unabii wao wenyewe lakini maneno haya hayakuweza kusaidia watu wakati walipohitaji kusaidiwa (mash. 1-5). Manabii hawa walisema unabii wao ilitoka kwa Bwana, lakini ulikuwa uwongo (mash. 6-7). Wataharibiwa kwa sababu ya kutangaza salama wakati salama ilipokosa, na kwa sababu ya kupakaa ukuta na chokaa wakati ukuta huu ulipokuwa karibu kuanguka (mash. 8-16). Manabii wanawake walifanya uchawi na kushona hirizi juu ya viko vyaa mkono na kufunika vichwa vyao na vitambaa. Walijaribu kuua watu wengine na uchawi wao na

14 EZEKIELI

waliacha wengine hai. Mungu ataokoa watu wake na kuharibu wanawake hawa waovu (mash. 17-23).

Manabii wanawake walijaribu kuua watu namna gani?

SURA 14

Wengine wa wazee wa watu walikuwa wakiabudu sanamu kwa siri. Walifika karibu na Ezekieli na kutenda sawasawa walitaka kujua mapenzi ya Mungu. Bwana alitangaza ya kwamba atajibu waabudaji sanamu hawa ye ye mwenyewe, si kwa njia ya nabii. Kama nabii akijibu waabudaji sanamu hawa, atadanga-nywa, na Mungu atamhukumu pamoja na watu wale walioabudu sanamu kwa siri (mash. 1-11) .

Noa, Danieli na Yobu walikuwa watu wa Mungu kabisa. Hata kama watu hawa waliombea waabudaji sanamu, Mungu hatawasikia. Atatuma taabu kwa watu na watateswa na njaa, nyama wakali, vita na tauni (mash. 12-20). Mungu ataleta maneno haya juu ya taifa lo lote linalofanya zambi; atafanya hivi zaidi sana na Yerusalema pahali hekalu lake liliposimamishwa, pahali ilipopasa watu kujua ya kwamba haifai kuabudu sanamu! Hata hivi Mungu ataokoa watu wachache watakaoweza kutoa ushuhuda ya kwamba Mungu alitenda kwa haki wakati alipofanya maneno haya (mash. 22-23) .

Viongozi wa Yerusalema walifikiri Mungu atasahau zambi zao kwa sababu walikuwa wazao wa Abrahamu na Isaka. Ezekieli aliwaambia ya kuwa hata watu wanaotembea karibu sana na Bwana hawawezi kuokoa watu wengine. Vijana wengi wanafikiri wao ni Wakristo kwa sababu wazazi wao ni Wakristo. Biblia inatufundisha ya kwamba inapasa kila mtu kupokea Kristo kuwa Mwokozi wake mwenyewe.

Noa, Danieli na Yobu waliweza kuponyesha watu wangapi?

SURA 15

Watu wa Yerusalema walikuwa kama mzabibu. Mzabibu una faida kwa neno moja tu, ndilo kuzaa matunda. Kuni za mzabibu si namna ya kuni za miti mingine na hazitoshi kwa kazi ya kufanya meza au viti. Na kama kuni za mzabibu zikichomwa kwa moto, faida yao inapunguka hata kupita. Watu wa Yuda

hawakuzaa matunda kwa Mungu na kwa sababu hii wata-chomwa kwa moto wakati Wababeli watakapofika kupiga vita na wenyeji wa Yerusalem (mash. 1-8).

SURA 16

Ndani ya sura hii Bwana alipasha habari za huzuni za Yerusalem kama mfano kwa watu wote wa Yuda. Alisawanisha Yerusalem kwanza na mtoto msichana mchanga, na nyuma yake na msichana mkubwa. Kwanza Yerusalem ulikuwa kama mtoto mchanga ambaye mama yake hakutaka kumzaa wala kumwosha kwa maji (mash. 1-5). Bwana alimhurumia na kumlinda na mapendo (mash. 6-7). Mtoto alipata nguvu na kugeuka msichana mkubwa na Bwana alimwoa na kumpa vitu vingi (mash. 8-14). Lakini watu wa Yerusalem waliacha Bwana na waliabudu sanamu. Walikuwa kama mke anayegeuka kahaba (mash. 15-22). Walifanya uasherati na mataifa mengine vilevile. Kwa pahali pa kutegemea Bwana waliomba mataifa hawa kuwasaidia (mash. 23-29). Ni desturi kwa kahaba kutaka mshahara, lakini Yerusalem ulikuwa namna nyingine—ulilipa watu wengine waweze kuzini nao (mash. 30-34). Mungu atauharibu pamoja na mataifa ambalo ulilipa (mash. 35-43). Zambi za kuogopesha za Yerusalem na Yuda ziliwu mbaya kupita zambi za Wahiti, Waamori, Samaria na Sodomo (mash. 44-52). Lakini Mungu atatendea Sodomo na Samaria na Yerusalem kwa neema; miji hii itajengwa tena na kugeuka miji mikubwa kwa wakati wa kuja (mash. 53-58). Atafanya agano la milele na watu wake na watu wa Yuda watakuwa na haya kwa sababu walikwenda mbali na Bwana kwa kuabudu sanamu (mash. 59-63).

Ni lazima kwa Mungu kuhukumu taifa lo lote linalokwenda mbali naye. Wakati watu wengine wanapomwona akifanya hivi, neno hili lingepasa kuwa maonyo kwao waachane na zambi zao na kugeuka kwa Mungu. Ingetupasa sisi kufanya vivyo.

Kwa njia gani Yerusalem ulikuwa kama mke mwovu?

SURA 17

Mungu aliagiza Ezekieli kuwaambia Wayuda mezali juu ya tai na mizabibu. Tai mkubwa alivunja kitawi kidogo kilichokuwa juu

16 EZEKIELI

sana cha mwerezi na kukipeleka kwa inchi ya mbali. Tai huyu alikamata vilevile mbegu ya inchi na kuipanda ndani ya udongo mzuri. Mbegu iliota na kugeuka mzabibu ulioenea juu ya udongo (mash. 1-6). Halafu mzabibu ulianza kuotesha matawi yake kuelekana tai mwingine lakini haukuota tena vizuri (mash. 7-10). Ezekieli alieleza mezali hii ndani ya mashairi 11-21. Tai wa kwanza alikuwa Nebukadneza, mfalme wa Babeli (sh.12). Alipeleka Yoyakinu, mfalme wa Yuda (tawi lililokuwa juu zaidi) toka Yerusalem (Lebanoni) hata Babeli (inchi ya biashara) na kwa mji Babeli (ndio mji wa wenyewe kufanya biashara). Alikamata Zedekia vilevile (mbegu ya inchi) na kumsimamisha kama mfalme wa Yuda (sh.13; 2 Wafalme 24:12-13,17). Kwa muda mfupi Zedekia aliendelea vizuri kama mfalme wa Yuda, lakini nyuma aligeuka, akaomba mfalme wa Misri (tai mkubwa mwingine) kusaidia kuokoa Yuda toka mikono ya Wababeli (2 Mambo 36:13; Isaya 30:1-2). Kwa sababu hii Zedekia atapelekwa kwa Babeli na atakuifa pale (mash. 16-21). Alivunja mapatano yake na Nebukadneza; neno hili lilikuwa kama kuvunja ahadi iliyotolewa kwa Mungu (sh.19). Ndani ya mashairi 22-24, Mungu aliahidi ya kwamba Masiya, *tawi dogo* lingine, atakuja. Atakuwa mzao wa jamaa ya Daudi. Atakuwa mti mwenye kuzaa matunda mengi na watu watakaa na salama chini ya matawi yake (sh.23).

SURA 18

Watu wa Yuda walikuwa na mezali iliyosema walikuwa waki-testwa kwa sababu ya zambi za baba zao (mash. 1,2). Mungu alibisha neno hili na alisema inapasa kila mtu kujibu Mungu juu ya zambi zake mwenyewe (mash. 3,4). Halafu Mungu alionyesha namna anavyohukumu watu:

1. Mtu anayetembea kwa haki ataishi (mash. 5-9).
2. Mwana mwovu wa mtu mwenye haki atakuifa (mash. 10-13).
3. Mwana mwenye haki wa mtu asiye haki ataishi (mash. 14-17), lakini baba asiye haki atakuifa (sh.18).
4. Mtu mwovu ataishi kama akiacha zambi zake (mash. 21-23).
5. Mtu wa haki anayetenda zambi atakuifa (sh.24).

Watu walikaa kushitaki Mungu kusema hatendi kwa haki laki-ni Mungu aliwaonyeshea ya kwamba yeche ni mwenye haki kwa

sababu hata mtu mwovu anaweza kuokolewa kama akiachana na zambi zake, na hili ndilo neno Bwana analotaka wafanye (mash. 25-32).

Usifikiri mashairi haya yanageuza mafundisho ya Kutoka 20:5. Ndani ya Kutoka tunajifunza ya kwamba watoto wa mtoto wa mtu na watoto wao vilevile watateswa hapa duniuni kwa sababu ya zambi za baba wa baba wao. Roho Mtakatifu anatufundisha ndani ya Ezekieli 18 ya kuwa Mungu ataazibu mtu mwenye zambi tu na ni lazima kwake kufa kwa zambi zake. Ni sharti kwa kila mtu kubeba hukumu yake mwenyewe.

Watu wengine wanashitaki wazazi wao kwa matata yote wanayopata. Neno hili si taratibu. Ni lazima kwa kila mwanamume na kila mwanamke, kila kijana na msichana, kujibu Mungu wakati anapoulizana naye juu ya matendo yake. Mtu akirudi tena kwa Mungu, Mungu atamsamehe. Haya ndiyo mafundisho ya sura 18.

Ni. lazima kwangu kutenda zambi kwa sababu baba na mama wangu ni wenyewe zambi?

SURA 19

Sura hii ni wimbo wa huzuni kwa wafalme wa mwisho wa Yuda. Walimu wengine wa Biblia wanafikiri Ezekieli alikuwa akisema juu ya Yoahazi, Yoyakimu na Zedekia, watatu wa wafalme wane wa mwisho waliotawala katika Yerusalem. Kabilia la Yuda linaitwa simba mke. Makabilia mengine yanaitwa simba na watawala wao wana-simba (sh.2). Labda mtoto wa simba aliyegeuka mwana-simba (sh.3) ni mfano wa Yoahazi aliyefungwa na kupelekwa kwa Misri (sh.4). Labda mtoto mwingine wa simba ni Yoyakimu, lakini walimu wengine wanafikiri ni Yoyakinu. Ndani ya shairi 9 tunaona mwana-simha huyu akipelekwa kwa Babeli kama mfungwa. Mama ndani ya shairi 10 ni Yerusalem uliokuwa mzabibu wenyewe kuzaa matunda mengi kwa wakati wa mbele. Ulikuwa na wafalme wa nguvu (magongo) mbele lakini Wababeli (upepo wa mashariki) watauharibu na watu wake watapelekwa pahali pengine (jangwani) kama wafungwa (mash. 11-14).

SURA 20

Wazee wa Israeli walifika karibu na Ezekieli tena na kusema

18 EZEKIELI

walitaka Mungu kuwaongoza. Bwana alijua mafikiri yao na alikataa kuwajibu. Aliwakumbusha ya kwamba Waisraeli walikuwa wamemwasi tena na tena:

1. Waliabudu sanamu katika inchi ya Misri (mash. 4-8); Mungu hakuwaazibu kwa wakati ule kusudi watu wa Mataifa wasipate njia kucheka jina la Mungu (sh.9).
2. Hawakushika siku za sabato jangwani kama Mungu ali-
vyoagiza (mash. 10-13). Mara hii vilevile Mungu haku-
waonyeshea gazabu yake kwa sababu ya watu wa mataifa
(mash. 14-17).
3. Watu hawa walikuwa wamekaa ndani ya inchi ya Misri
lakini watoto wao walikwenda mbali na Bwana vilevile
(mash. 18-21). Mara hii vilevile Mungu aliwaachilia (mash.
22-26).
4. Mungu aliwaleta kwa inchi aliyoahidi kuwapa, lakini pale
vilevile Waisraeli waliabudu sanamu na walitoa hata wana
wao kama zabihu (mash. 27-31).

Watu wa Israeli walijaribu kuwa sawasawa na mataifa mengine lakini Mungu hakukubali neno hili kuendelea kwa siku nydingi (sh.32). Atawakusanya tena toka inchi pahali walipokuwa wafungwa na kuwasimamisha mbele yake kwa hukumu. Atapokea watu wenye haki na ataazibu waovu (mash. 37,38). Taifa la Israeli watarudishwa kwa inchi yao na hawataabudu sanamu tena. Kisha wataabudu Bwana kwa utakatifu (mash. 39-44).

Ndani ya Biblia iliyoandikwa zamani kwa Kiebrania shairi 45 la sura 20 ni mwanzo wa sura 21. Ndani ya mashairi 45-49 kuna unabii wa hukumu juu ya Yuda na Yerusalem; wataharibiwa kama miti wakati mwitu unapoteketezwa. Ni mfano wa majeshi ya Wababeli watakaokuja kupigana na watu wa mji.

Ezekieli aliwaambia watu waziwazi ya kwamba Mungu atawahukumu kwa zambi zao. Watu hawakutaka kusikia maneno haya, hivi walitenda sawasawa hawakufahamu (sh.49). Walikataa kuamini ya kwamba Mungu alikuwa akiwaonya.

Mungu alirehemu Israeli mara nydingi. Basi Mungu hata wahukumu kamwe?

SURA 21

Ndani ya mashairi 1-7 Mungu alisema ya kwamba ataharibu Yuda na Yerusalem. Ezekieli alihuzunishwa sana wakati alipoonya watu juu ya azabu kali ambayo Mungu atawaazibu nayo. Wanaume wa Babeli walikaa na panga zao tayari kwa uuaji (mash. 8-13). Wataharibu wenye zambi nyingi kufika wakati gazabu ya Mungu itakapokwisha (mash. 14-17). Ndani ya mashairi 18-24 tunaona mfalme wa Babeli akikaribia inchi na akifikia njia-panda. Njia moja ilikwenda kwa upande wa Yerusalem na njia nyingine kwa upande wa Rabati, mji mkubwa zaidi wa Waamoni. Mfalme atapiga vita na mji gani kwanza? Aliomba roho wabaya kumwongoza kwa njia tatu: (1) alitwaa mishale miwili na kuandika juu ya mshale mmoja Yerusalem na juu ya mshale wa pili Rabati; (2) aliuliza sanamu za miungu yake mwenyewe; na (3) aliangalia ndani ya maini ya nyama aliyechinjwa. Kisha alichagua kupiga vita na Yerusalem kwanza. Zedekia ndiye yule mkubwa mwovu wa Israeli ndani ya shairi 25. Alikuwa mfalme lakini hatakuwa na amri tena. Ndiyo, alikuwa mfalme wa mwisho wa watu wa Mungu kufika kuja kwa Masiya. Itakuwa haki ya Masiya kutawala (mash. 25-27).

Nyuma yake mfalme wa Babeli atapiga vita na Waamoni na kuwaharibu kabisa (mash. 28-32).

SURA 22

Ndani ya mashairi 1 kufika 12 zambi mbalimbali za watu wa Yerusalem zinatajwa: walimwanga damu kwa njia ya kutoa watoto kama sadaka; waliabudu sanamu (mash. 3,4); waliua watu (sh.6); walizaraau wazazi wao; walikuwa na ukali kwa wageni, kwa watoto waliofiwa baba zao, na kwa wajane (sh.7); walichafua hekalu na kuchafua siku za sabato (sh.8); walisema wongo na kuabudu sanamu juu ya milima (sh.9). Walitenda uzini, hata na watu wa jamaa zao wenyewe (mash. 10,11); waliua watu kwa bei, walikopesha mali na kula riba kubwa zaidi, NA walisahau Mungu (sh.12). Kwa zambi hizi zote Mungu atawasambaza katikati ya mataifa (mash. 13-16). Yerusalem utakuwa kama chungu ambacho mtu anatumika nacho kuyeyusha chuma juu ya moto mkali, aweze kuondosha sehemu ya chuma isiyo na faida. Mungu alisema watu wa Israeli walikuwa kama vyuma mbalimbali

20 EZEKIELI

visivyo na faida (mash. 17-22). Watu namna zote walikuwa na kosa machoni mwa Bwana: manabii (mash. 25,28); makuhani (sh.26); viongozi wa mji (sh.27); na watu wote (sh.29). Mungu alitafuta watu wa haki, lakini hata mmoja hakupatikana (mash. 30,31).

Kwa nini Mungu alisema watu wa Israeli walikuwa kama vyuma mbalimbali?

SURA 23

Sura hii ni mfano wa ndugu wanawake wawili waliokuwa makahaba, Ahola na Aholiba. Ahola alikuwa mfano wa Samaria na Aholiba alikuwa mfano wa Yerusalem (mash. 1-4). Ahola alikuwa kahaba wa Waasuria ambao walimpenda, vijana wa kutamaaniwa waliotembea juu ya farasi. Basi Mungu aliacha Ahola mikononi mwa watu wale nao walirnwua (mash. 5-10). Aholiba alikuwa hata mbaya kuliko ndugu yake. Aliabudu sana-mu na alifanya uasherati hata kupita Ahola. Kwanza alipenda picha za watu wa Babeli, kisha alituma wajumbe kuwaita kufikia inchi yake. Alikumbuka zambi alizofanya wakati alipokuwa inchini mwa Misri na alijitoa mzima kwa watu wa Babeli kwa kutenda uasherati (mash. 11-21). Basi Mungu atatumika na Wababeli ambao walimpenda kwa kumharibu. Wanaume wale ambao aliwataka sana sana watamtendea kwa ukali (mash. 22-35). Ndugu wale wawili wote walitenda uasherati na uuaji na walitoa watu kama sadaka (sh.37). Walichafua hekalu na kuvunja sabato (sh.38); waliabudu sanamu pamoja na kuabudu Bwana vilevile (sh.39); walifanya uasherati kwa njia ya kufanya maagano na mataifa mengine kwa pahali pa kutegemea Bwana (mash. 40-44). Mungu atachagua watu wenye haki wa mataifa mengine kuazibu ndugu wanawake hawa (ndio Samaria na Yerusalem) na kuwararibu (mash. 45-49).

SURA 24

Ezekieli alipasha mezali ya sufuria iliyotokota siku adui walipoanza kupiga vita na watu wa Yerusalem. Sufuria ilikuwa mfano wa Yerusalem; vipande vya nyama vilikuwa mfano wa watu. Sufuria ilikuwa karibu na kutokota. Kulikuwa na kutu ndani yake, mfano wa zambi kubwa ya watu, ndiyo kuabudu sanamu. Vyote vilivyokuwa ndani ya sufuria vitamwangwa na

sufuria lenyewe litateketezwa kuondosha uchafu wenyewe. Neno hili lilikuwa mfano wa namna Mungu atakavyojaribu kulazimisha watu wake kuacha kuabudu sanamu (mash. 1-14). Mungu alijulisha Ezekieli ya kwamba mke wake ("tamaa ya macho yako") atakuifa na alimkataza kuombolea au kutoa machozi (mash. 15-18). Watu waliomba Ezekieli kuwaelezea maana ya matendo yake. Alisema nao ya kwamba haifai wahuzunishwe wakati Mungu atakapoharibu *tamaa ya macho yao*, ndilo hekalu, na wakati wana wao na binti wao watakapouawa (mash. 19-24). Ni kama mashairi 25-27 yanafundisha ya kwamba Mungu hakutaka Ezekieli kutabiri tena kwa watu wa Yuda kufika wakati aliposikia ya kwamba adui zao walikuwa wamekamata mji.

Kwa nini Mungu alikataza Ezekieli kutoa machozi wakati mke wake alipokufa [sh.17]?

SURA 25

Ndani ya sura 25-32 tunasoma namna Mungu atakavyohukumu mataifa saba waliokuwa wapagano. Taifa la kwanza lilikuwa Amoni. Waamoni walifurahi wakati Nebukadneza aliposhinda Yerusalem na kupeleka watu wengi kwa Babeli kama wafungwa, hivi Wababeli (watu toka mashariki) watawaharibu vilevile (mash. 1-7). Taifa la pili lilikuwa Moabu. (Haifai Seiri kutajwa ndani ya shairi 8.) Wababeli watakamata inchi yao vilevile. Maneno yaliyopata Waamoni yatapata Wamoabu vilevile (mash. 8-11). Taifa la tatu lilikuwa Edomu. Waedomu watahukumiwa kwa sababu walilipiza Yuda kisasi (mash. 12-14). Taifa la ine lilikuwa Filistia. Mungu atawaazibu kwa sababu walikuwa adui za watu wa Yuda tangu zamani (mash. 15-17).

SURA 26

Fungu la tano la watu watakaohukumiwa na Mungu walikuwa watu wa Tiro. Mji huu ulikuwa kando ya bahari. Tunasoma juu ya azabu yao ndani ya sura 26, 27 na kufika shairi 19 la sura 28. Watu wa Tiro walifurahi wakati waliposikia adui za Yuda walikuwa wamekamata Yerusalem. Walifikiri watapata biashara yote ya mji wa Yerusalem vilevile sasa (mash. 1,2). Mungu alisema atatumika na mataifa mengi kuazibu watu wa mji huu. Unabii ndani ya mashairi 4-6 umetimizwa kabisa. Kwanza Nebukadneza alipiga vita na Tiro (mash. 7-11), lakini watu wa

22 EZEKIELI

Tiro walikimbia na vitu vyao vyote, wakakwendea kisanga kidogo karibu na pwani. Jina la kisanga hiki ni Tiro vilevile. Walikaa pale na salama kwa miaka 250. Kisha mfalme mwingine, Alesanduro Mkubwa, alitengeneza njia kufikia kisanga hiki kwa njia ya kutupa mabomoko ya Tiro wa kwanza baharini (mash. 12-14). Mataifa mengine wataogopa sana wakati watakaposikia ya kwamba Tiro ulikuwa umeharibiwa (mash. 15-21). Kama Mungu alivyosema ndani ya shairi 21, mji huu haukusimamishwa tena.

Alesanduro aliharibu mji wa Tiro. Ulijengwa tena wakati gani?

SURA 27

Mashairi 1-9 yanatujulisha ya kwamba mji wa Tiro ulikuwa kama merikebu nzuri sana. Ulijengwa na vitu vya bei ya damani vilivyoletwa toka pahali pote duniani. Ndani ya mashairi 10 na 11 tunasoma juu ya askari za Tiro. Watu wa mji huu walifanya biashara na makabila mengi mengine (mash. 12-26a). Lakini upepo wa mashariki (mufano wa Wababeli) utaharibu muji wao (mash. 26b,27). Watu wa mataifa mengine watashangaa sana wakati watakaposikia habari hizi (mash. 28-36) .

SURA 28

Mukubwa wa Tiro alikuwa mwenye kiburi na akili, na alikuwa mutajiri (mash. 1-6) ; lakini Wababeli walimuharibu hata hivi (mash. 7-10). Yeye ni mufano wa mupinga Kristo. Ona 1 Yoane 2:22; 2 Watesalonika 2:3-10. Mufalme wa Tiro alijulikana kwa sababu alikuwa mutu wa kuonekana vizuri sana, lakini aliharibiwa kwa sababu ya kiburi yake kubwa. Walimu wengi wa Biblia wanafikiri ya kwamba mashairi 11-19 yanatupasha habari za kuanguka kwa Shetani toka mbinguni.

Fungu la sita la watu Mungu atakaowahukumu walikuwa watu wa muji wa Sidoni. Sidoni ulikuwa kando ya bahari, karibu na Tiro. Mungu alionya watu wa Sidoni ya kwamba wengi wao watapata ugonjwa na kufa, na wengine watauawa vitani, lakini hakusema ya kwamba muji wao utaharibiwa kwa milele (mash. 20-23). Mji wa Sidoni ungali kwa wakati wa sasa, lakini Tiro umeharibiwa kabisa (ona 26:21). Mashairi 24-26 yanatupasha ya kwamba taifa la Israeli litasimama tena na kubarikiwa wakati Bwana atakaposimamisha ufalme wake duniani.

Ndani ya shairi 2 Ezekieli alisema na mkubwa wa Tiro na ndani ya shairi 12 na mfalme wa Tiro. Mkubwa wa Tiro alikuwa mtu, lakini aligeuka mwenye kiburi kabisa, hata alijiita Mungu. Ni kama Roho Mtakatifu aliongoza Ezekieli kusema juu ya Shetani aliyekuwa akiongoza mkubwa mwovu wa Tiro. Shetani alikuwa kwa Edeni (sh.13). Mungu aliumba Shetani na kumweka kama kerubi au malaika kwa pahali pa heshima (sh.14), lakini zambi na kiburi zilioneekana ndani ya Shetani na Mungu alimfukuza. Tumeona ya kwamba Shetani alitaka kuwa sawasawa na Mungu (Isaya 14:13-14). Shetani ni adui wa Mungu hata sasa na anachukia watu wa Mungu. Haifai kwetu kuogopa Shetani lakini kushindana naye. Tukifanya hivi atatuacha (Yakobo 4:7; (1 Petro 5:8,9).

Mkubwa wa Tiro ni mfano wa nani? Mfalme wa Tiro ni mfano wa nani?

SURA 29

Taifa la saba litakalohukumiwa na Mungu lilikuwa Wamisri (29:1 – 32:32). Ni kama Mungu atawahukumu kupita mataifa yote mengine.

Farao alikuwa kama mamba aliyekaa ndani ya Mto Nili. Samaki zilikuwa mfano wa Misri. Mungu alisema atawahukumu wote. Watu wa Israeli walikuwa wameomba Wamisri kuwasaidia, lakini Wamisri hawakuweza kuwasaidia hata kidogo (mash. 6-9a). Mungu ataacha inchi ya Misri kwa miaka 40 kwa sababu ya kiburi ya Farao (mash. 9b-12). Nyuma yake atakusanya watu wa Misri tena lakini Misri hautakuwa tena kamwe ufalme mkubwa kama mbele, na watu wa Israeli hawataomba Wamisri tena kamwe kuwasaidia (mash. 13-16). Nebukadneza alikuwa amesumbuka sana kukamata mji wa Tiro lakini hakupata mshahara kwa kazi yake kwa sababu watu walikimbia kwa kisanga pamoja na vitu vyao vyote. Kwa sababu hii Mungu atampa inchi ya Misri kama mshahara wake (mash. 17-20). Ni nguvu kufahamu maana ya shairi 21. Kama “siku ile” ndiyo siku iliyotajwa ndani ya 24:27, halafu ni siku adui watakapokamata mji wa Yerusalem. Kwa wakati ule nabii atawezu kutabiri juu ya Yuda tena.

SURA 30

Wababeli watashinda Wamisri na adui zao zote (mash. 1-9). Nebukadneza ndiye atakayeharibu vitu vyote inchini mwao (mash. 10-12). Ndani ya mashairi 13-19 tunaona majina ya miji mikubwa zaidi ya Misri itakayoharibiwa: Nofi, Patro (tunafikiri mji huu ulikuwa kwa upande wa kusini wa Misri), Soani, No, Sini, Aweni, Pibeseti na Tehafunesi. Mashairi 20-26 yanatonyeshea ya kwamba Misri haikuharibiwa yote mara moja. Mungu alivunja mkono mmoja wa Farao kwanza wakati adui zake walipomshinda kwa vita ya Karkemesi. Alivunja mkono wake wa pili wakati Wababeli walipoingia Misri na kuishinda.

Mungu alivunja mikono ya Farao kwa sababu gani?

SURA 31

Farao alifanana na nani wakati alipokuwa mfalme mkubwa? Alifanana na mfalme wa Asuria. Mfalme huyu alikuwa na uwezo mkubwa. Alikuwa mkubwa kupita wafalme wote wengine, kama mwerezi ulio mrefu kupita miti yote mingine (mash. 1-9). Lakini Mungu alisaidia Wababeli kushinda mfalme wa Asuria (mash. 10-14). Alishushwa chini kabisa hata Hadeze (kaburi) mbele ya macho ya mataifa mengine (mash. 15-17). Farao alikuwa kama mfalme huyu wa Asuria. Aligeuka mkubwa lakini ataharibiwa na kushushwa chini hata Hadeze (sh.18).

SURA 32

Farao alifikiri alikuwa kama simba, lakini Mungu alimwita joka wa bahari na alisema atamkamata ndani ya wavye wake na kumharibu. Mfalme wa Babeli ataharibu vitu vyote ambavyo watu wa Misri walijivuna juu yao na inchi itabaki kimya na bule (mash. 1-16). Watu wa Misri watatumwa kwa Hadeze. Ndani ya mashairi 17-31 tunaona kama pahali pale ni namna gani. Watu wa Asuria ni pale (mash. 22,23), na watu wa Elamu (mash. 24,25), wa Meseki na Tubali (mash. 26-28), wa Edomu (sh.29), na wa Sidoni (sh.30). Taifa la Misri lilikuwa taifa kubwa hapa duniani, lakini kwa Hadeze litakuwa na haya sawasawa na mataifa yote mengine (mash. 31,32).

Huu ndio mwisho wa unabii wa Ezekieli juu ya mataifa haya saba.

Misri ni mfano wa dunia iliyo adui ya watu wa Mungu. Haifai tupende dunia na furaha zake. Tukipenda Mungu hatutapenda dunia (1 Yoane 2:15-17).

SURA 33

Kuanza na sura hii kufika hata mwisho wa kitabu hiki Ezekieli alipasha zaidi ya kwamba watu wa Israeli watarudi karibu na Mungu na kujenga hekalu tena.

Ndani ya sura hii Ezekieli ni kama zamu: ni lazima kwake kuonya watu juu ya zambi zao. Wataharibiwa kama wakikataa kunyenyeka maonyo yake lakini neno hili halitakuwa kosa la Ezekieli. Kama zamu asipoonya watu, watu wenyewe watakuwa lakini Mungu ataa zibu zamu kwa sababu ya kufa kwao (mash. 1-9).

Watu walinungunika na kusema Mungu hakuwatendea kwa haki, lakini Mungu alisema neno hili si kweli. Aliwakumbusha ya kwamba atasamehe mtu mwovu anayekiri na kuacha zambi zake. Ataa zibu vilevile mwenye haki anayeanza kutenda mabaya (mash. 10-20). Ezekieli aliweza kusema tena nyuma ya kusikia ya kwamba Yerusalem ulikuwa umeharibiwa (mash. 21-22; ona 24:27).

Ni kama mashairi 23-29 yanatupasha juu ya Wayuda wachache waliobaki kwanza inchini nyuma ya kuharibiwa kwa Yerusalem. Walisema Abrahamu alikuwa mtu mmoja tu lakini Mungu alimpa inchi hii. Walisema wao walikuwa watu wengi na walifikiri walikuwa na ruhusa kusema ya kwamba inchi hii ilikuwa inchi yao. Mungu alisema neno kubwa si kama walikuwa watu wangapi lakini kama walitembea namna gani. Hata kwa wakati ule walikuwa wakiabudu sanamu na itakuwa sharti kwa Mungu kusafisha inchi kwa njia ya kuondosha uovu ule wote. Watu walipenda kusikia masemo ya Ezekieli lakini hawakutaka kuyatii. Watajua ya kwamba nabii alikuwa katikati yao wakati masemo yake yatakapotimizwa (mash. 30-33).

Ndani ya sura 1 na 2 Ezekieli aliona ono kubwa la kwanza. Nyuma yake Mungu alisema naye kuonya watu namna inavyopasa askari mlinzi kufanya (sura 3). Ezekieli alionya watu wa Yuda na ukali kabisa (sura 4-24), lakini walikataa kutubu. Basi Mungu alitoa Yerusalem na hekalu kwa Wababeli. Ezekieli aliuzunishwa sana juu ya neno hili. Labda alifikiri kazi yake ilikuwa

26 EZEKIELI

yote bule. Tunaona ya kwamba hapa ndani ya sura 33 Mungu alisema na Ezekieli namna alivyosema naye ndani ya sura 3. Watu walikataa kutubu lakini ilipasa Ezekieli kukaa kuwaonya. Inatupasa sisi kufanya vivyo hivyo na kujulisha watu wote wa dunia ya kwamba Mungu anawapenda na ya kuwa Kristo aliwakufia.

Mungu ataazibu zarnu kwa sababu gani?

SURA 34

Wachungaji (watawala wa Israeli) walijifikiri wenyewe tu na hawakusaidia kondoo (watu) vizuri. Walitawala bila mapendo na kondoo walisambazwa (mash. 1-6). Kwa sababu hii Mungu ali-fanya shauri kuponyesha kondoo zake toka wachungaji hawa wabaya (mash. 7-10). Yeye atakuwa Mchungaji wao –Mchungaji mwema –na atawarudisha tena kwa inchi yao na kutawala juu yao kwa wakati wa utawala wa Kristo duniani kwa miaka elfu moja (mash. 11-16). Ataponyesha vilevile kondoo zake za kweli toka mikono ya wachungaji wabaya walio wenyewe jeuri na wanaojifikiri wenyewe tu (mash. 17-24). Mtumishi wangu Daudi ndani ya mashairi 23 na 24 ndiye Bwana Yesu aliye mzao wa Daudi. Mashairi 25-31 yanaonyesha ya kwamba kondoo watacaa na salama na watakuwa na vitu vyote watakavyohitaji wakati Bwana Yesu Kristo atakapotawala dunia.

Bwana Yesu alijiita Mchungaji Mwema. Wote walikuja mbele yake walikuwa wachungaji wa uwongo. Alitoa uzima wake kwa ajili ya kondoo zake naye ni hai tena na anawalinda (Yoane 10:8,11,28).

SURA 35

Mlima Seiri ni jina lingine kwa inchi ya Edomu. Bwana alisema atahukumu inchi ile kwa sababu Waedomu walichukia Wayuda tangu zamani na walifurahi wakati Yerusalem ulipoharibiwa. Walitendea na ukali Wayuda waliokimbia na walikusudi kukamata inchi ya Israeli wao wenyewe. Basi inchi ya Edomu itaharibiwa na kuachwa kwa milele.

SURA 36

Watu wameita sura hii *Habari Njema ya Ezekiel*, zaidi kwa sababu ya mashairi 25-30.

Adui za Waisraeli walisema maneno mabaya juu yao na wali-fanya shauri kukamata inchi yao, lakini Mungu yeye mwenyewe atarudisha watu wake kwa inchi yao (mash. 1-7). Watu watakaa tena ndani ya miji na vijiji. Watasitawi, inchi yao itazaa matunda mengi, na watu wa mataifa mengine hawatasema maneno mabaya juu yao tena (mash. 8-15).

Mungu atabariki inchi na kurudisha watu wake waweze kukaa ndani yake tena (mash. 16-38). Walikuwa wafungwa ndani ya inchi nyingine kwa sababu walikuwa wameua watu wengi na kuabudu sanamu. Watu wa mataifa mengine walisema maneno mabaya sana juu ya Mungu kwa sababu ya zambi za watu wake (mash. 16-21). Mungu atarudisha Waisraeli kwa inchi yao watu wasiseme maneno haya mabaya tena, si kwa sababu Waisraeli walistahili kurudi. Atawasafisha na atawapa moyo mpya na roho mpya (maana yake watazaliwa tena). Matunda na vyakula vitakomea vizuri kupita mbele na watu hawatateswa na njaa tena kamwe. Bwana atafanya maneno haya yote kwa sababu yeye ni mwenye neema, si kwa sababu Waisraeli walistahili kubarikiwa hivi (mash. 22-32). Mataifa kando kando ya Israeli watajua ya kwamba Mungu alirudisha watu wake kwa inchi yao wailime tena na kupanda vyakula (mash. 33-36). Kwa wakati ule kutakuwa na wanaume wengi katika Yerusalema sawasawa na hesabu ya makundi kwa siku kubwa kama Pasaka (mash. 37,38). Unabii huu ulitimizwa kwa sehemu wakati Wayuda waliporudi toka inchi ya Babeli. Utatimizwa kabisa kwa wakati wa kuja, ndio wakati Bwana Yesu Kristo atakapotawala juu ya dunia.

Bwana Yesu alisema na Nikodemo ingalimpasa kujua mbele ya kwamba ni sharti kwa watu kuzaliwa tena (Yoane 3:10). Hapa ndani ya Ezekiel 36:26 Mungu aliahidi kuwapa watu moyo mpya na roho mpya. Soma 11:19 na 18:31 tena.

Namna gani ninaweza kupata moyo mpya na safi?

SURA 37

Ndani ya ono la mashairi 1 na 2 Ezekiel aliona mifupa ya kukauka ya Israeli na Yuda ndani ya bonde. Mungu alimwigiza kutabiri kwa mifupa ile nayo itapata uzima tena. Hivi Ezekiel aliisema Neno la Mungu mara ya kwanza, na mifupa ilifunikwa

na nyama na ngozi (mash. 7,8). Alisema tena na halafu pumzi ili-ingia ndani yao (mash. 9,10). Maneno haya yalikuwa mfano kuonyesha ya kwamba Bwana atarudisha taifa la Israeli kwa inchi yao na karibu na Mungu wao tena (mash. 11-14).

Halafu Mungu aliagiza Ezekieli kukamata miti midogo miwili. Mti mmoja ulikuwa mfano wa Yuda, na wa pili ulikuwa mfano wa Israeli walioitwa Yosefu hapa au Efuraimu. Alishika miti miwili na miisho yao kugusana hata ilionekana kama mti mrefu mmoja. Taifa la Israeli lilitengwa miaka 345 mbele kuwa falme mbili kwa wakati wa Mfalme Rehoboamu, na mfano huu wa miti ulionyesha ya kwamba falme hizi mbili zitakuwa ufalme mmoja tena. Mfalme mmoja (ndiye Masiya) atatawala juu yao nao wataokolewa na kusimamishwa tena (mash. 15-23). Daudi (ndiye Bwana Yesu Kristo) atakuwa Mfalme, na watu watamtii. Mungu atafanya agano la salama nao, ndilo agano la milele, na watakuwa na hekalu tena (mash. 24-28). Unabii huu haujatimizwa bado.

Mungu atakutanisha makabila 12 ya Israeli tena na kuwarudisha kwa inchi yao ya mbele. Bwana Yesu atakuja kwanza kwa Kanisa lake; kisha atakuja tena kutawala juu ya Israeli na dunia nzima.

Mungu aliagiza Ezekieli kusema na mifupa ya kukauka kwa sababu gani?

SURA 38

Sura hii na sura 39 zinatujulisha namna gani Mungu ataharibu watu wale watakuwa adui za Israeli kwa wakati wa kuja. Gogi ndiye kiongozi wa adui hawa na Magogi ndilo jina la inchi yake. Watu wanaojifunza Biblia sana hawapatani ndani ya mafikiri yao kama Gogi ni nani. Ni kama maneno haya yatatokea nyuma ya kurudi kwa Waisraeli kwa inchi yao na mbele ya kuja tena kwa Kristo duniani.

Mungu atawapa Gogi na rafiki zake hamu kutayarisha majeshi yao kwa vita (mash. 1-6). Watakwenda kwa kusini kupigana na Israeli. Wayuda watafikiri hakuna hatari hata kama wakikaa ndani ya miji isiyo na kuta (mash. 7-16). Halafu majeshi ya Gogi yatajaza inchi. Mungu atakuwa na wivu juu ya watu wake na atakasirika sana hata atapigana na adui zao. Kutakuwa na tete-meko kubwa la inchi. Gogi na watu wake wataogopa sana wakati

Mungu atakapowapiga na ugonjwa mbaya sana na wengi wao watakufa. Mungu atanywesha moto juu yao vilevile na kutuma tufani kubwa (mash. 17-23).

SURA 39

Majeshi makubwa ya Gogi yataharibiwa kabisa juu ya milima ya Israeli (mash. 1-6). Toka siku ile hakuna mtu atakayesema neno bayo juu ya jina takatifu la Mungu tena (mash. 7-8). Silaha za askari za Gogi zitasambazwa pahali pote milimani. Watu wa Israeli watatumika nazo kama kuni kwa moto kwa miaka saba (mash. 9-10). Kazi ya kuzika maiti itakula miezi saba, zitazikwa ndani ya bonde la Hamoni-Gogi kwa upande wa mashariki wa Bahari ya Chumvi (mash. 11-16).

Ndege na nyama za mwitu watakula maiti—itakuwa kama karamu kwao (mash. 17-20). Siku ile mataifa watajua ya kwamba Waisraeli walikuwa wafungwa mbele kwa sababu ya zambi zao wenyewe, si kwa sababu Mungu alikuwa zaifu na hakuweza kushinda adui zao (mash. 21-24). Waisraeli watarudi karibu na Bwana kweli. Watasahau haya yao na watakiri ya kwamba Mungu ni Bwana wao (mash. 25-29).

Mungu anakaa juu ya kitu chake cha kifalme siku zote naye ni juu ya maneno yote. Ataruhusu adui za Waisraeli kuja kupigana nao lakini atawaharibu wakati saa yao itakapotimia.

Nani atakuwa kiongozi wa jeshi kubwa la adui za Israeli kwa wakati wa kuja?

SURA 40

Ndani ya sura 40-42 tunasoma maneno mengi juu ya hekalu ambalo Wayuda watajenga kwa Yerusalem. Maneno mengi ndani ya sura hizi ni nguvu kufahamu, lakini mengine ni wazi.

Ndani ya mashairi 1-4 Ezekieli alikuwa na ono la mji wa Yerusalem na la hekalu kwa wakati wa utawala wa Kristo duni-ani kwa miaka elfu moja. Aliona viwanja viwili, kimoja ndani ya kiwanja cha pili.

Shairi 5 — ukuta wa kiwanja cha inje cha hekalu.

Mash. 6-16 — lango la mashariki la kiwanja hiki cha inje.

Mash. 20-23 — lango la kaskazini la kiwanja cha inje.

30 EZEKIELI

Mash. 24-27 – lango la kusini la kiwanja cha inje. (Hatusomi neno juu ya lango la mangaribi.)
Mash. 28-31 – lango la kusini la kiwanja cha ndani.
Mash. 32-34 – lango la mashariki la kiwanja cha ndani.
Mash. 35-37 – lango la kaskazini la kiwanja cha ndani.
Mash. 38-43 – meza kwa pahali pa kuingia lango la kaskazini pahali wanapoweza kuchinja sadaka za nyama.
Mash. 44-47 – Vyumba kwa malango ya kaskazini na kusini kwa makuhani.
Mash. 48 na 49 - pahali pa kuingia hekalu.

Ni wazi ya kwamba hekalu la Mungu litajengwa tena katika Yerusalem. Ezekieli alikuwa ameonya watu wa Yuda ya kuwa Mungu ataharibu hekalu lililojengwa na Mfalme Solomono. Sasa Mungu alionyeshea Ezekieli ono la hekalu jipya, la ajabu kabisa litakalojengwa wakati Bwana Yesu atakapokuja tena. Mungu anatimiza ahadi zake kila mara.

Mungu alimpa Ezekieli ono la hekalu jipya miaka mingapi nyuma ya kuharibiwa kwa hekalu la Solomono?

SURA 41

Ndani ya sura 40 tulisoma juu ya viwanja vilivyozunguka hekalu. Sura 41 inatupasha habari za hekalu lenyewe.

Mash. 1 na 2 – pahali patakatifu pa hekalu.
Mash. 3 na 4 – pahali patakatifu sana.
Mash. 5-11 – vyumba 30 kwa kila daraja la hekalu. (Kulikuwa na dari tatu.)

Shairi 12 – jengo kwa upande wa mangaribi wa hekalu.

Mash. 13-15a – vipimo vya hekalu na vya viwanja ambavyo vilivizunguka.

Mashairi 15b-26 – vitu vilivyokuwa ndani ya hekalu.

SURA 42

Mashairi 1-14 - Vyumba vya makuhani kwa upande wa kaskazini na kusini wa hekalu, na kazi yao.

Mashairi 15-20 - Vipimo vya kiwanja cha inje.

Leo Kanisa la Mungu ni hekalu lake duniani. Anakaa ndani yetu; Roho Mtakatifu anakaa ndani ya miyo yetu (Waefeso 2:19-22).

SURA 43

Ndani ya shairi 23 la sura 11 tuliona wingu la utukufu liki-ondokea hekalu kwa Yerusalem polepole. Lakini utukufu wa Mungu utarudi tena kwa njia ya Bwana Yesu wakati atakapokujja kutawala (mash. 1-5). Atakaa kwa milele katikati ya watu wake nao hawataabudu sanamu tena karibu na hekalu (mash. 6-9). Hekalu litasimama juu ya mlima mmoja na Mungu alisema kichwa kizima cha mlima huu kitakuwa kitakatifu sana (mash. 10-12). Ndani ya mashairi 13-17 tunaona kipimo cha mazabahu itakayojengwa. Ni kama itajengwa kwa sehemu tatu, moja juu ya nyingine. Kila sehemu itakuwa ndogo kupita sehemu iliyo chini yake. Ndani ya mashairi 18-27 Mungu alisema na Ezekieli nini itawapasa kufanya wakati watakapoanza kutumia mazabahu hii mpya.

Bwana Yesu Kristo ataleta utukufu wake kwa hekalu hili litakalojengwa katika Yerusalem kwa wakati wa kuja. Leo Mwana wa Mungu anakaa ndani ye-tu. Huu ndio utukufu wa Kanisa. Haifai tujitafutie wenyewe utukufu. Inatupasa kutenda yaliyo mema watu waweze kuona utukufu wa Bwana ndani yetu.

Wingu la utukufu litarudia hekalu la Mungu wakati gani?

SURA 44

Sharti langa la mashariki la kiwanja cha inje lifungwe wakati wote kwa sababu Masiya ataiingia kwa langa hili wakati atakaporudi kwa hekalu lake na hatatoka tena kamwe. Mkubwa tu atawenza kukaa kwa pahali pa kuingia hekalu (mash. 1-3). Ni kama mkubwa huyu ni mzao wa Daudi atakayetawala chini ya Kristo, Mfalme.

Watu wa inchi nyingine hawatatumika kazi tena ndani ya hekalu (mash. 4-8). Walawi walitumikia sanamu kwa wakati watakuwa na ruhusa kufanya kazi hii (mash. 9-14). Wana wa Zadoki watafanya kazi ya makuhani (mash. 15,16). Itawapasa kuвая mavazi ya kitani (mash. 17-19), na kutii maagizo mengine

vilevile (mash. 20-27). Watapewa vitu vyote watakavyohitaji kwa maisha yao ya kila siku (mash. 28-31).

SURA 45

Katikati ya inchi ya Israeli, sehemu ya inchi itawekwa mbali kwa Bwana kama sadaka. Sehemu ndefu ya sehemu ile itakuwa kwa Pahali Patakatifu Sana na kwa makuhani (mash. 3-4). Hekalu litakuwa pale, ndipo pahali watu watakapoabudu Mungu (sh.2). Sehemu nyingine itakuwa kwa Walawi (sh.5). Sehemu hizi mbili zote zinaitwa takatifu.

Chini ya toleo takatifu (ndiyo sehemu ya inchi iliyowekwa mbali kwa Bwana) kutakuwa na sehemu ndefu nyingine ya udongo, ndiyo sehemu ya tatu. Sehemu hii haitakuwa takatifu na mji wa Yerusalem utasimama juu yake (sh.6).

Udongo kwa upande wa mashariki na mangaribi wa inchi hii na kufika hata mipaka ya inchi utakuwa mali ya mkubwa (mash. 7-8).

Mungu aliagiza wakubwa kutenda kwa haki (sh.9). Haifai wadanganye watu wakati wanaponunua au kuuza vitu (mash. 10-12). Ndani ya mashairi 13-17 tunaona ya kwamba ni lazima kwa watu kumpa mkubwa sehemu ya mavuno yao kwa sadaka ya siku zote. Mungu anataka hekalu kusafishwa siku ya kwanza ya mwezi wa kwanza (mash. 18,19), na watu siku ya saba ya mwezi ule ule (sh.20). Itawapasa kula Pasaka siku ya kumi na ine ya mwezi wa kwanza (mash. 21-24), na kushika siku kubwa ya vibanda siku ya kumi na tano ya mwezi wa saba (sh.25).

Waisraeli watacaa ndani ya inchi ya Palestina wakati Kristo atakaporudi kama Mfalme kutawala kwa miaka 1000 (Ufunuo 20:4). Watu watashika sheria za Musa na kutoa zabihu kwa Mungu. Mbele ya kuja kwa Kristo zabihu za Waisraeli zilitazama mbele kwa Kalvari. Waamini kwa wakati wa sasa ni ndani ya Kanisa nao si chini ya sheria ya Musa na hawatoi sadaka za nyama. Wakati Bwana atakapokuja tutakuwa pamoja naye kwa milele.

Kwa nini Waisraeli watatolea Mungu zabihu za nyama wakati Kristo atakapokuja tena kutawala?

SURA 46

Ndani ya mashairi 1-8 Mungu alionyesha namna gani anataka mkubwa kuingia kiwanja cha inje na pahali gani itakapompassa kusimama wakati atakapoleta matoleo yake kwa karamu ya sabato na ya siku ya kwanza ya mwezi. Haifai watu watoke kiwanja cha inje kwa lango lile walipoingia. Kwa mfano, kama waliingga kwa lango la kaskazini itawapasa kutoka kwa lango la kusini (mash. 9,10). Mashairi 11 na 12 yanapasha juu ya matoleo ya mkubwa, na mashairi 13-15 juu ya zabihu itakazopasa watu kutolea Bwana kila siku. Bwana alitoa sheria kusudi mkubwa asiweze kupoteza mali yake bila kuipata tena na ili hataweza kungeza juu yake kwa njia isiyo haki (mash. 16-18). Kutakuwa na pahali kuhani atakapoweza kupika matoleo (mash. 19-20), na ndani ya kiwanja cha inje kutakuwa na pahali kwa kutokotesha zabihu za watu (mash. 21-24).

SURA 47

Ezekieli aliona ndani ya ono mto uliotoka kwa mlango wa hekalu. Mto huu ulipita kwa mazabahu, toka ukuta wa kusini wa lango la mashariki, na kufika hata Bahari ya Chumvi (inayoitwa vilevile Bahari ya Kufa). Utasafisha maji ya bahari na halafu kutakuwa na samaki wengi baharini (mash. 1-12).

Nyuma yake tunasoma juu ya mipaka ya inchi kwa wakati ule (mash. 13-20), na kama watu watagawa inchi namna gani. Makabila ya Israeli wataigawa katikati yao kwa njia ya kupiga kura na wageni watakaokaa katikati yao watapata nusu yake vilevile (mash. 21-23).

Ezekieli aliona mto ambao unatuleta kufikiri juu ya mto wa uzima (Ufunuo 22:1). Hata leo sisi tuna oamin tunaweza kuleta maji ya uzima kwa watu wengi (Yoane 7:38).

Maji yatakayotoka hekalu yatapita wapi?

SURA 48

Ni kama inchi itatengwa kwa sehemu ndefu nyembamba toka mpaka wa mangaribi hata mpaka wa mashariki. Sehemu kwa upande wa kaskazini wa inchi itakuwa ya kabile la Dani (sh.1). Kabilal la Aseri litakuwa kwa upande wa kusini wa kabile la Dani

(sh.2); nyuma yake makabila ya Nafutali (sh.3), Manase (sh.4), Efuraimu (sh.5), Rubeni (sh.6), na Yuda (sh.7). Kwa upande wa kusini kwa Yuda itakuwa sehemu ya inchi iliyoletwa kwa mku-bwa. Ndani ya sehemu hii ni hekalu na mji wa Yerusalem (mash. 8-22). Kabilia la Benyamina litakuwa kwa upande wa kusini wa inchi iliyo ya mkubwa (sh.23), nyuma yake Simeoni (sh.24), Isakari (sh.25), Zebuluni (sh.26), na Gadi (sh.27). Mji Yerusalem utakuwa na malango 12, matatu kwa kila upande. Jina lake litakuwa Yehova-shama, maana yake Bwana ni pale.

Roho Mtakatifu ametuonyeshea maneno machache juu ya Yerusalem mpya na inchi ya Israeli. Neno la ajabu zaidi ni ndani ya shairi la mwisho la unabii huu, ndilo hili: *Bwana ni pale*. Ameahidi kuwa pamoja nasi vilevile, hata kama tukiwa watu wawili au watatu tu tunaokutana pamoja (Matayo 18:20). Ameahidi kuwa pamoja na watu wale vilevile wanaotii agizo lake kwenda na kuhubiri habari zake kwa watu wengine (Matayo 28:20).

Jina jipya la Yerusalem litakuwa nini?

DANIELI

SEHEMU KUBWA

Sura

- 1 Danieli na rafiki zake walikaa waaminifu kwa Mungu.
- 2 Nebukadneza, mfalme wa Babeli, aliota ndoto juu ya sanamu iliyofanywa toka vyuma namna ine.
- 3 Nebukadneza alifanya sanamu ya zahabu na kutupa Wayuda watatu ndani ya tanuru ya moto kwa sababu walikataa kuinama mbele ya sanamu yake.
- 4 Nebukadneza aliota ndoto juu ya mti uliokatwa na Danieli alimwelezea maana ya ndoto hii.
- 5 Mungu alijulisha Belsasari ya kwamba atakufa. Habari hizi ziliandikwa juu ya ukuta na Danieli alijulisha mfalme maana ya maandiko yenye.
- 6 Dario, mfalme wa Persia aliagiza watu wote kuomba kwake tu kwa siku 30. Alitupa Danieli ndani ya pango la simba kwa sababu aliomba Mungu.
- 7 Danieli aliota ndoto juu ya nyama wakali wane. Nyama hawa walikuwa mfano wa falme au mataifa mane watakaotawala dunia.
- 8 Danieli aliota ndoto juu ya beberu na mbuzi ndume. Nyama hawa walikuwa mifano ya mataifa mawili.
- 9 Mungu alijulisha Danieli ya kwamba mataifa mengine watatawala juu ya watu wa Israeli kwa majuma 70 (ndiyo miaka 70).
- 10 Danieli aliona utukufu wa Mungu, na Mungu alimwonyeshea maneno mengine yatakayotokea kwa wakati wa kuja.
- 11,12 Mungu alijulisha Danieli tena maneno mengine yatakayotokea kwa wakati wa kuja.

A. Maneno yatakayotokea nyuma kidogo, 11:1-35.

- 1) Wayunani watashinda majeshi ya Medo-Persia, 11:1-3.
- 2) Taifa la Wayunani litaharibika, 11:4-35.
 - a) Wamisri watapiga vita na Wasuria, 11:4-20.
 - b) Maneno maovu Antioko Epifanesi atakayofanya wakati atakapokuwa mfalme, 11:21-35.

B. Maneno yatakayotokea nyuma ya wakati mrefu, 11:36-12:13.

- 1) Mtu mmoja atashindana na Kristo na atasema yeze mwenyewe ni Kristo, 11:36-45.
- 2) Kutakuwa na wakati wa taabu na mateso makubwa sana, 12:1-13.

Nebukadneza aliyeleka Danieli pamoja na Wayuda wengine kwa Babeli kama wafungwa. Yoyakimu alikuwa mfalme wa Yuda kwa wakati ule; ndio karibu rniaka 606 B. C. [mbele yu kuzaliwa kwa Kristo duniani].

Nebukadneza alimpa Danieli kazi ya heshima katika serikali na Belsasari alifanya vivyo hivyo nyuma yake.

Dario alishinda Wababeli vitani na alifanyiza Danieli mtu mwenye amri kupita watu wote ndani ya ufalme wake ila yeze mwenyewe. Danieli alikuwa na kazi ya heshima vilevile wakati Kiro alipokuwa mfalme.

Maana ya jina la Danieli ni "Mungu ni Mwamuzi wangu." Unabii wa Danieli ni zaidi juu ya maneno yatakayotokea wakati mataifa mengine watakapotawala juu ya Wayuda. Alipasha habari za mataifa wane watakapotawala dunia. Watatawala Wayuda vilevile. Nyuma yake Danieli alipasha juu ya wakati Kristo atakapotawala na kuvunja uwemo wa mataifa yale mengine.

SURA 1

Sura hii inatujulisha habari za maneno yaliyotokea katika Babeli nyumbani mwa mfalme. Mfalme Nebukadneza aliagiza watumishi wake kutayarisha wanaume vijana wa Israeli kwa kazi ya kutumikia mfalme na kumsaidia na mashauri mema. Kati yao Danieli, Hanania, Misaeli na Azaria walichaguliwa kwa kazi hii, lakini walipewa majina mapya kwa lugha ya Wakaldea: Beltesaza, Sadiraki, Mesaki na Abedenego. Mfalme aliwapa vyakula na mvinyo, namna aliyokula na kunywa yeze

mwenyewe. Labda vingine vyakula hivi vilikuwa namna Mungu alivyokataza Waisraeli kula; au labda vyakula hivi vili-tolewa kwa sanamu kwanza. Danieli alikuwa mhodari na alikataa kuvikula.

Ilikuwa nguvu kwa Danieli kukataa vyakula ambavyo mfalme alimpa, lakini alitaka kupendeza Mungu kupita mfalme. Ni lazi-ma kwetu kukataa maneno mengi kama tukitaka kupendeza Mungu. Sharti tukatae maneno yote yatakayotuzuiza tusitembee karibu na Bwana.

Danieli aliomba waweze kupewa mboga na maji kwa pahali pa vyakula na vinyweo vya mfalme (mash. 8-13). Mkubwa wa matowashi alikubali kufanya hivi. Nyuma ya wakati mfalme ali-waita na kuwapima. Vijana hawa walionekana vizuri kupita na walikuwa wenye akili kupita waganga na wachawi wote wa mfalme, hivi mfalme aliwaweka kuwa wasaidizi wake (mash. 14-21).

Kwa sababu gani Danieli alikataa kula vyakula mfalme alivyompa?

SURA 2

Nebukadneza aliota ndoto, lakini hakuweza kukumbuka ndoto yenewe wakati alipoamka asubui. Wachawi na wafumu wake hawakuweza kumkumbusha kama aliota nini, hivi Nebukadneza aliagiza askari zake kuua waakili wote, hata Danieli na rafiki zake vilevile (mash. 1-13). Danieli aliomba Mungu na Bwana alimjulisha kama mfalme aliota nini na maana ya ndoto yenewe (mash. 14-30).

Mungu alifunulia Danieli ndoto ya mfalme wakati Danieli na rafiki zake walipoomba. Mungu anaweza kusema nasi. Yeye ni tayari kusema na watu wote wanaotaka kufanya mapenzi yake na kuishi kwa yeye.

Ndani ya ndoto yake mfalme aliona sanamu ya mtu mwenye kichwa cha zahabu, na kifua na mikono ya feza. Tumbo lake na viuno vyake vilikuwa vya shaba. Miguu yake ilifanywa vya chuma. Halafu nyayo za miguu yake zilikuwa machanganyiko ya chuma na udongo.

Mfalme aliona vilevile jiwe lililochongwa toka mwamba pasipo kazi ya mikono. Jiwe hili liliangukia sanamu na kuivunja.

Nyuma yake ukubwa wa jiwe hili ulikaa kuongezeka kufika wakati lilipokuwa mlima mrefu na kujaza dunia nzima (mash. 31-35) .

Sanamu ilikuwa mfano wa mataifa mane watakaotawala juu ya dunia nzima na juu ya Wayuda. Kichwa cha zahabu kilikuwa mfano wa Nebukadneza na taifa la Babeli. Sehemu iliyokuwa ya feza ilikuwa mfano wa ufalme wa Yunani na miguu ilikuwa mfano wa taifa la Roma. Jiwe lilikuwa mfano wa Bwana Yesu. Atavunja na kuharibu mataifa yale mane na kutawala yeye mwenyewe juu ya dunia nzima (mash. 36-45). Nebukadneza aliona ya kwamba Danieli alikuwa mwenye akili kabisa na alimfanyiza mtawala wa inchi nzima ya Babeli. Rafiki watatu wa Danieli waligeuka wasaidizi wake (mash. 46-49).

*Mungu alionyeshea Nebukadneza nini ndani ya ndoto
yake ya kwanza?*

SURA 3

Nebukadneza alifanya sanamu kubwa sana yenye urefu kwenda juu wa karibu mètres 30, na aliagiza watu kuinama mbele yake na kuiabudu wakati waliposikia sauti ya mziki. Alisema wale wasioinama watatupwa ndani ya moto mkali kabisa (mash. 1-7). Sadiraki, Mesaki na Abednego walikuwa Wayuda walio-fuata Mungu na uaminifu, hivi walikataa kuinama mbele ya sanamu. Kulikuwa na watu wengine ambao waliwachukia na watu hawa walikwenda kuwashitaki karibu na mfalme. Walisema Wayuda hawa watatu walikataa kuinama mbele ya sanamu (mash. 8-12). Mfalme aliwapa njia kugeuka na kuinama mbele ya sanamu yake lakini walikataa. Basi mfalme aliagiza watumishi wake kuongeza ukali wa moto na kuwatupa ndani (mash. 13-21). Moto ulikuwa mkali sana hata uliuu watu wale waliotupa Wayuda ndani yake. Nebukadneza alishangaa sana wakati alipoangalia ndani ya moto. Aliona wanaume wane ndani ya moto, Wayuda wale watatu na mtu mmoja mwininge aliye-onekana kama Mwana wa Mungu (mash. 22-25). Moto hauku-umiza Wayuda hata kidogo; uliteketeza tu kamba ambazo ziliwafunga mbele. Mfalme alifikiri neno hili ndilo ajabu kabisa, na toka siku ile alikataza watu kusema neno baya tena juu ya Mungu wa Wayuda. Aliwapa Wayuda wale watatu kazi ya heshima kupita mbele ndani ya serikali yake (mash. 26-30).

Mara moja moja Mungu anafanya ajabu namna hii kwa watu kuona. Tunasoma juu ya mara hii moja tu ya kwamba aliponyesha watu waliotupwa ndani ya tanuru ya moto. Hata hivi anafanya maneno mengi ya ajabu kwa watu wake ambao wanaomfuata na uaminifu. Labda watu wengine hawajui habari za maneno ya ajabu Mungu aliidotutendea, lakini maneno haya yanatusaidia kumsifu na kumwamini kupita mbele.

Rafiki watatu wa Danieli walikataa kutii agizo la mfalme kwa sababu gani?

SURA 4

Ndani ya sura hii Nebukadneza alipasha habari za neno ambalilimpata na kumsaidia kugeuka kwa Mungu wa kweli (mash. 1-3). Aliota ndoto na watu wake wenye akili hawakuweza kumjulisha maana yake, hivi aliita Danieli na kumwambia habari za maneno aliyoota (mash. 4-8). Ndani ya ndoto yake aliona mti mzuri sana wenye matunda mengi. Mti huu ulikuwa mkubwa na mrefu sana. Halafu mtakatifu alishuka toka mbinguni, akasema sharti mti ukatwe lakini kisiki cha shina lake kiliachwa katika udongo (mash. 9-15). Nyuma yake Nebukadneza aliota juu ya mtu aliyegeuka kama wazimu, kama nyama ya mwitu kwa miaka saba (mash. 16-18). Danieli alijulisha mfalme ya kwamba mti ulikuwa mfano wake (yeye Nebukadneza) na utawala wake juu ya inchi zote za dunia. Lakini kwa miaka saba hatakuwa na mammaka na akili yake itapotea. Atakuwa kama nyama ya mwitu. Ndani ya ndoto kisiki cha shina la mti kiliachwa udongoni. Neno hili lilionyesha ya kwamba Nebukadneza hatakuwa lakini atageuka mfalme tena (mash. 19-26). Mfalme alisikia habari hizi lakini hakuona huzuni juu ya zambi zake, hivi nyuma ya mwaka mmoja maneno aliyoota yalifanyikana. Alikaa kama nyama ya mwitu kwa miaka saba, lakini mwishoni aligeuka kwa Mungu, akasema Mungu ni mkubwa na anakaa milele. Kisha Nebukadneza alikuwa mfalme tena.

Maana ya ndoto ya pili ya Nebukadneza ilikuwa nini?

SURA 5

Belsasari alikuwa mwana wa Nabonidus aliyejukwa mwana wa Nebukadneza. Tunasoma ndani ya shairi 2 ya kwarnba

Nebukadneza alikuwa baba yake, lakini kwa Agano la Kale maana nyingine ya neno hili "baba" ni baba ya baba. Belsasari alifanya karamu kubwa na kutumia sahani Nebukadneza alizoiba toka hekalu kwa Yerusalem (mash. 1-4). Halafu wakati wakubwa wale walipokuwa wakikunywa na kuchekacheka, mkono ulionekana na kuandika maneno juu ya ukuta. Malkia alisema Danieli atawenza kueleza maana ya maandiko yenyewe, hivi mfalme alituma mtu kumwita (mash. 5-16). Danieli alikumbusha mfalme habari za maneno yaliyopata Nebukadneza. Alisema na Belsasari ya kwamba ilikuwa vibaya kwa yeze kunywa mvinyo kwa karamu yake toka kopo za hekalu la Yerusalem (mash. 17-24).

Andiko juu ya ukuta lilisema ya kwamba Mungu hataruhusu Wababeli kutawala tena. Lilisema vilevile ya kuwa Mfalme Belsasari hakufanya maneno ambayo ilimpasa kufanya na Mungu atawapa Wamedi na Wapersi ufalme wake. Haya ndiyo maneno yaliyoandikwa: MENE, MENE, TEKELI UFARSINI. Maana ya MENE ni *kuhesabiwa*. Mungu alikuwa amehesabu ufalme wa Babeli na kuumaliza. Maana ya TEKELI ni *kupimwa*. Mungu alikuwa amepima Belsasari na aliona ya kwamba Belsasari hakufikia kipimo Mungu alichotaka. Maana ya UFARSI-NI ni *kugawanyika*. Usiku ule ule majeshi ya Wamedi na Wapersi waliingia mji wa Babeli na kuua Belsasari. Dario aligeuka mfalme wa inchi zote Belsasari alizozitawala mbele. Ufalme wa Babeli uligeuka ufalme wa Persia.

Mungu alisema nini na Belsasari?

SURA 6

Dario alikuwa mfalme wa Wamedi na Wapersi na alifanyiza Danieli mtu mkubwa zaidi katika serikali yake (mash. 1-3). Wengine wa maakida ya mfalme walichukia Danieli, hivi waliomba mfalme kutoa amri kusema sharti watu waombe kwa mfalme tu, si kwa mungu yo yote. Dario alitoa amri hii mpya na halafu hakuna mtu aliyezeza kuigeuza (mash. 4-9). Danieli alikaa kuomba Mungu mara tatu kila siku kama mbele na adui zake walikwenda mbio kumshitaki kwa mfalme (mash. 10-13). Dario alijaribu sana kusaidia Danieli, lakini hakuweza kugeuza sheria aliyofanya na ilimlazimisha kutupa Danieli ndani ya pango la

simba (mash. 14-17). Mfalme aliogopa simba wataua Danieli lakin ni asubui aliona ya kwamba hawakumwumiza hata kidogo. Basi aliagiza adui za Danieli watupwe ndani ya pango la simba na simba waliwaua na kuwakula mara moja. Kisha Dario alitoa amri nyingine kusema sharti watu wote waheshimu Mungu wa Danieli (mash. 18-28).

Mungu alikaa kuchunga watu wake Wayuda hata wakati walipokuwa wafungwa inchini mwa Babeli. Wengi wa watu wake walikaa kumfuata hata kwa Babeli na walionyesha kwa mataifa mengine ya kuwa Bwana ni Mungu mkubwa, Mungu hai. Mungu alilinda vijana watatu wakati walipokuwa ndani ya tanuru ya moto, na Nebukadneza, mfalme wa Babeli, aliona ya kwamba Mungu ni mkubwa, Mungu wa ajabu. Mungu alilinda Danieli asiawe na simba, na Dario, mfalme wa Wamedi na Wapersi, aliona vilevile kwamba Mungu ni mkubwa, Mungu wa ajabu.

Kwa nini mfalme alitia mhuri kwa pango pahali Danieli alipotupwa?

SURA 7

Ndani ya sura 1-6 za kitabu cha Danieli tunasoma habari za maneno yaliyotokea kwa wakati ule ule. Ndani ya sura 7-12 tunasoma juu ya maneno yatakayotokea nyuma. Danieli aliandika sura 7 na 8 kwa wakati Belsasari alipokuwa mfalme wa Babeli, mbele ya wakati wa utawala wa Wamedi na Wapersi.

Danieli aliota ndoto na aliona nyama mbalimbali wane ndani ya sura 7. Nyama hawa walikuwa mifano ya mataifa mane waliotawala dunia. Simba alikuwa mifano wa **Babeli**. Dubu alikuwa mifano wa **Wamedi na Wapersi**. Dubu alishika mifupa mitatu ya mbavu ndani ya kinywa chake; labda mifupa hii ilikuwa mifano wa miji mikubwa mitatu ndani ya inchi ya Babeli iliyoaribiwa na Wamedi na Wapersi wakati Kiro alipokuwa mfalme wao. Chui alikuwa mifano wa Yunani. Vichwa vine vya simba ni mifano wa sehemu ine za ufalme wa Yunani nyuma ya kufa kwa Alesanduro mkubwa. Nyama wa ine ni mifano wa taifa la **Roma**. Pembe kumi ni mifano ya inchi kumi waliotawaliwa na Waroma.

Danieli alitabiri juu ya ufalme wa tano utakaotawala dunia

42 DANIELI

nzima kwa siku za mwisho (sh.9). Mungu yeye mwenyewe atampa Bwana Yesu amri kutawala dunia nzima.

SURA 8

Nyuma ya miaka miwili Danieli aliona nyama ndume wawili ndani ya ndoto. Kondoo ndume alikuwa mfano wa inchi ya Persia (sh.20), beberu alikuwa mfano wa inchi ya Yunani (sh.21). Alesanduro mkubwa alipigana na majeshi ya Wapersi na kuwashinda, lakini inchi yake ilitengwa kwa sehemu ine nyuma ya kufa kwake (sh.8). Danieli aliona pembe ndogo juu ya kichwa cha beberu. Pembe hii ni mfano wa mfalme wa sehemu moja ya ufalme wa Yunani, Antioku Epifanesi. Alizuiza Wayuda wasi-abudu Bwana kwa Yerusalem. Nyuma ndani ya sura hii pembe ile ndogo ni mfano wa mtu atakayekuwa na uwezo mkubwa kwa siku za mwisho. Atakuwa mkali kabisa, na mwenye hasira, na atapigana na Bwana, anayeitwa Mkubwa wa wakubwa, na Bwana atamwua (mash. 23-25).

Ndani ya sura 2, sanamu ni mfano wa mataifa makubwa mane na ndani ya sura 7 na 8 nyama wakali ni mifano ya mataifa. Andika majina ya nyama walio mifano ya mataifa yale, na andika vilevile jina ya kila taifa.

Danieli 2	Danieli 7	Danieli' 8	Jina la Taifa
Zahabu	_____	_____	_____
Feza	_____	_____	_____
Shaba	_____	_____	_____
Chuma na udongo	_____	_____	_____

SURA 9

Maneno tunayosoma ndani ya sura hii yalitokea wakati Dario, mfalme wa Wamedi, alipotawala. Danieli alisoma kitabu cha Yeremia polepole na aliona ya kwamba ile miaka 70 ilikuwa karibu kwisha. Hii ndiyo hesabu ya miaka watu wa Yuda waliyokuwa wafungwa katika Babeli (mash. 1-2). Danieli alikiri mbele ya Mungu ya kwamba yeye na watu wa Yuda walikuwa

wamefanya zambi na aliomba Bwana kufanya kwa Yerusalem na watu wa Yuda maneno aliyoahidi kuyafanya (mash. 3-19).

Malaika Gabrieli alimfikia wakati alipokuwa akiomba na alimjulisha mengine ya maneno yatakayopata watu wa Yuda kwa muda wa majuma makumi saba. Maana ya juma moja ndiyo miaka saba, hivi majuma saba ni miaka 490, tangu wakati mfalme wa Persia aliposema na Nehemia kujenga ukuta wa Yerusalem kufika wakati Bwana Yesu atakapokuwa Mfalme katika Yerusalem. (Majuma 69 ya majuma yale 70 yamepita na wakati wa sasa ni muda unaotangulia kuanza kwa juma la makumi saba. Hatujui wakati gani juma hili la mwisho litakapoanza.)

Kutakuwa na majuma saba (miaka 49) na majuma 62 (miaka 434), yote miaka 483 toka wakati mfalme alipoagiza Wayuda kujenga Yerusalem kufika wakati Kristo alipokuja mara ya kwanza (sh.25). Masiya alikufa juu ya msalaba kwa zambi za watu nyuma ya kupita kwa miaka 434. Halafu Waroma waliharibu Yerusalem (sh.26). Nyuma yake kutakuwa na muda wa miaka fulani unaoitwa muda wa Kanisa. Muda huu haujawkisha bado.

Maneno tunayosoma ndani ya shairi 27 hayajatokea bado. Kwa juma la makumi saba, ndiyo miaka saba ya mwisho ufalme wa Waroma utakuwa na uwezo mkubwa tena. Mtawala wake atatenda kama rafiki ya Wayuda, lakini hatatimiza ahadi atakazotolea Wayuda, na halafu Wayuda watateswa sana kwa miaka mitatu na nusu. Bwana Yesu Kristo atakuja tena, ataazibu adui zake na ataanza kutawala katika Yerusalem kwa mwisho wa miaka mitatu na nusu.

Tunasoma maneno mengine ya ajabu ndani ya sura hizi za Danieli. Zilijulisha watu wazi kabisa maneno mengi yatakayotokea nayo yalitokea kweli namna Mungu alivyomwambia Danieli. Mengine ya maneno haya hayajatokea bado lakini tunajua bila shaka ya kwamba yatafanyikana vilevile namna Danieli alivysema. Bwana Yesu Kristo atakuja na kutawala juu ya dunia nzima.

Danieli alisoma ndani ya Kitabu cha Mungu ya kwarnba Waisraeli watakuwa wafungwa katika Babeli kwa miaka 70. Mungu alimjulisha habari za majuma 70 ya miaka. Miaka hii 490 itakwisha wakati gani?

SURA 10

Maneno tunayosoma ndani ya sura hii yalitokea mwaka wa tatu wa utawala wa Kiro kama mfalme wa Persia. Kiro alikuwa ameruhusu Wayuda kurudi kwa inchi yao, lakini Danieli alibaki kwa Babeli. Alikuwa amelia kwa Mungu kwa majuma matatu. Alikuwa akisimama kando ya mto Hidekeli wakati Mungu alipotuma malaika karibu naye ambaye alimwambia kwa nini Mungu hakujibu maombi yake mbele. Roho mbaya alikuwa amezuiza mjumbe wa Mungu. Roho huyu alitawala mioyo ya watawala wa Persia (sh.13). Malaika aliahidi kujulisha Danieli maneno yatakayopata Wayuda kwa siku za mwisho (sh.14). Alimwambia Danieli maneno haya ndani ya sura 11 na 12. Halafu malaika alisema atakwenda kupigana kwanza na mkubwa wa Persia na nyuma yake na mkubwa wa Uyunani (sh.20).

Kwa nini malaika alikawa mda mrefu mbele ya kujibu maombi ya Danieli?

SURA 11

Maneno tunayosoma ndani ya mashairi 1-35 yanakwisha kutokea. Maneno ndani ya mashairi 36-45 yatatokea kwa wakati wa kuja. (Lakini maneno ndani ya mashairi 1-35 yalikuwa haya-jatokea bado wakati Danieli alipoandika juu yao.)

Mashairi 1-35 yanapasha juu ya uwezo wa wafalme wane wa Persia na juu ya kushindana kwa mfalme wa mwisho wa Persia na mfalme wa Uyunani (sh.2). Alesanduro Mkubwa alipigana na Wapersi na kuharibu uwezo wao hata hawakutawala juu ya watu wote wa dunia tena. Uyunani iligeuka inchi iliyotawala dunia nzima (sh.3). Halafu Alesanduro Mkubwa alikufa na wane wa wakubwa wake walitawala kila mtu juu ya sehemu moja ya ufalme wake (sh.4). Ndani ya mashairi 5-35 tunasoma juu ya vita na mfalme wa Misri, mfalme wa kusini, aliyepigana na Suria, mfalme wa kaskazini. Vita hizi ziliendelea kwa karibu miaka 200. Mashairi 21-35 yanapasha habari za Antioku Epifanesi, mfalme wa Suria. Aliharibu hekalu kwa Yerusalem na kulichafua.

Maneno tunayosoma ndani ya mashairi 36-44 yatatokea kwa wakati wa kuja. Mpinga Kristo ni kiongozi mkubwa atakayeshi-ndana na Kristo. Atasema yeeye ni Mungu na atafanya maneno makubwa na kusitawi kufika wakati gazabu ya Mungu juu ya

Israeli itakapokwisha (mash. 36-39). **Mfalme wa kaskazini** atafika kwa wakati wa kuja toka inchi ya Asuria. Atapigana na **mfalme wa kusini**, ndiye mfalme wa Misri, na atamshinda. Halafu atasikia habari za kuogopeshwa na ataanza kurudia inchi yake mwenyewe. Atasimama karibu na Yerusalem na kuuawa pale pamoja na jeshi lake.

SURA 12

Ndani ya shairi 1 tunasoma juu ya wakati wa taabu kubwa unoitwa **Mateso Makubwa**. Utaendelea kwa miaka mitatu mbele ya kurudi kwa Kristo duniani. Kristo atafufua watu wengine waliokufa nao watacaa pamoja na Kristo wakati anapotawala dunia. Bwana atatawala kwa miaka elfu moja na nyuma yake atafufua waovu wote na watahukumiwa kwa zambi zao (sh.2; Ufunuo 20:5).

Mungu aliagiza Danieli kuandika maneno haya ndani ya kitabu. Maana ya sehemu ya mwisho ya shairi 4 ni ya kama watu wengi watajifunza Biblia na kuifahamu vizuri kupita kwa wakati wa Mateso Makubwa yatakayoendelea kwa miaka 31/2, ndizo siku 1260. Labda **chukizo linaloleta ukiwa** litasimamishwa ndani ya hekalu la Mungu katika Yerusalem siku 30 **mbele** ya mwanzo wa Mateso Makubwa. Labda hii ndiyo maana ya siku **1290** ndani ya shairi 11. Shairi 12 linasema juu ya siku 1335. Labda hesabu hii inaongeza muda nyuma ya wakati Kristo atakapokwisha kuhukumu adui zake na mbele ya kuanza kutawala. Maana ya shairi 13 ni kusema Danieli atakufa au **kustarehe** na atapewa uzima tena (atasimama tena) na kuwa pamoja na Kristo wakati atakapotawala.

Ndani ya Agano la Kale Mungu hakupasha watu juu ya muda toka kufa kwa Kristo kufika wakati atakapokuja tena kutawala dunia nzima. Muda huu katikati ya kuja kwa kwanza na kuja kwa pili kwa Kristo unaitwa muda wa Kanisa. Kwa muda huu Mungu anaokoa mtu ye yote anayeamin Mwana wake, Bwana Yesu Kristo. Haazibu watu kwa zambi zao kwa wakati huu lakini anawaagiza kuzikiri na kuziacha na kuamini Bwana Yesu kuwa Mwokozi wao. Ametuagiza sisi kuwalishwa habari hizi. Bwana Yesu atakuja tena kutawala juu ya dunia nzima kwa mwisho wa muda huu.

Danieli aliagizwa kutia kitabu chake mhuri kufika wakati wa mwisho [sh.4]. Bwana Yesu alisema nini na Yoane katika Ufunuo 22:10?

MAJIBU - EZEKIELI

SURA

- 1 Alionyeshea Ezekieli ono la utukufu wake.
- 2 Yeremia na Yoane.
- 3 Mungu alimwagiza kuonya watu ya kama hatari ilikuwa karibu.
- 4 Kama alama kwa Israeli na Yuda (mash. 4,6).
- 5 Kama mfano kuonyesha ya kwamba Mungu atahukumu watu kwa njia mbalimbali.
- 8 Viongozi wa watu walikuwa wakiabudu sanamu pale.
- 9 Ndiyo. Zaidi ya watu walikuwa wameendelea sana ndani ya zambi yao, lakini kwanza malaika aliweka alama juu ya wale waliokuwa na huzuni.
- 11 Wakati Solomono alipomaliza kulijenga.
- 13 Kwa njia ya uchawi.
- 14 Waliweza kujiponyesha wenyewe tu (sh.14).
- 16 Watu wa Yerusalema walikwenda mbali na Bwana, waka-abudu miungu mingine na kuomba mataifa mengine kuwasaidia.
- 18 Hata tulipokea tabia ya zambi toka baba na mama zetu, Mungu atatuhukumu juu ya maneno sisi tunayofanya.
- 20 Hata Mungu alirehemu Israeli mara nyingi atawahukumu kwa wakati wa kuja, na watu wote wengine vilevile.
- 22 Mungu atawahukumu namna vyuma vinavyowekwa ndani ya moto kuvisafisha.
- 24 Mungu alitaka neno hili kuwa alama kwa watu kwa sababu mji wao na wana na binti zao wataharibiwa (sh.21).
- 26 Mji wa Tiro haukujengwa tena, kama Mungu alivyosema (sh.21) .
- 28 Wa Mpinga-Kristo; Shetani.
- 30 Neno hili ni mfano wa Mungu akiondolea Misri uwezo wake hata liligeuka taifa zaifu.

- 33 Atamwazibu kama akikosa kuonya watu ya kwamba hatari ni karibu.
- 34 Hawakuwapenda namna Mungu alivyowapenda.
- 36 Mungu tu anaweza kukupa moyo mpya na safi kama ukimwamini.
- 37 Ulikuwa mfano kuonyesha ya kwamba Israeli litakuwa taifa tena.
- 39 Gogi.
- 40 Mwaka wa kumi na ine (sh.1).
- 43 Wakati Bwana Yesu atakaporudia dunia tena.
- 45 Sadaka hizi zitatazama nyuma kwa mauti ya Kristo.
- 47 Yataingia bahari inayoitwa sasa Bahari ya Chumvi (sh.8).
- 48 Yehova-shama, kwa sababu Bwana atakuwa pale kwa milele (sh.35).

MAJIBU - DANIELI

Sura

- 1 Kwa sababu alikuwa amekusudi rohoni mwake ya kwamba hataasi sheria ya Mungu.
- 2 Ya kwamba Mungu alikuwa amemfanya mfalme wa dunia nzima, lakini wafalme wakubwa watatu wengine watamfuata.
- 3 Sheria ya Mungu iliwakataza kuinama na kuabudu mungu yo yote ila Mungu wa kweli.
- 4 Mungu alionyeshea mfalme ya kwamba atamwazibu kwa sababu ya kiburi yake, na nyuma yake atambariki tena.
- 5 Belsasari hakufanya mapenzi ya Mungu na ufalme wake utamwondolewa.
- 6 Ili wakubwa wasiweze kusema mfalme alifungua Danieli toka pango la simba.

8	Danieli 2	Danieli 7	Danieli 8	Taifa
	Zahabu	(Simba		Babeli
	Feza	(Dubu	Kondoo	Wamedi na
			ndume	Wapersi
	Shaba	(Chui	Beberu	Yunani
	Chuma na	(nyama mwenye		Roma
	udongo	pembe kumi		

48 **DANIELI**

- 9 Wakati Bwana Yesu Kristo atakaporudi na utukufu.
- 10 Kwa sababu roho mbaya alimzuiza.
- 12 Watu kwa wakati wa Danieli hawakuweza kufahamu kitabu chake vizuri, lakini sisi tunaweza kukisoma pamoja na kitabu cha Ufunuo, na Roho Mtakatifu atatusaidia kufahamu.